# Nipashe

Jumanne Septemba 3, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581788

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US





**SALAH: MSIMU HUU WA MWISHO KWANGU LIVER**

UKURASA 21

**Serikali** yafafanua madai ya JUKATA kupinga Uchaguzi Serikali za Mitaa

UKURASA 17

**Kigezo** umri ajira chazua mjadala bungeni

UKURASA 5

**Mambo** manne yatawala wagombea ubunge EALA

UKURASA 17

# Mabadiliko Sheria TAKUKURU

• **Faini** makosa rushwa ngono kuongezwa, kugusa uchaguzi, michezo kubahatisha... *Uk. 2*




Baadhi ya watoto waliookolewa kutoka kwenye utumikishwaji katika machimbo ya madini yaliyoko Kijiji cha Dilifu, Manispaa ya Mpanda, mkoani Katavi. **PICHA: MUSSA MWANGOKA**

# Sheria ya Madini kufumuliwa, biashara makinikia kurudishwa

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### WATANZANIA 80% KUFIKIWA NISHATI SAFI

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali imejipanga hadi kufikia mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania, watakuwa wanatumia nishati safi ya kupikia nyumbani ili kuepuka ukataji...

UKURASA WA 19

### MPOX YASAMBAA KILA KONA UGANDA

WIZARA ya Afya nchini Uganda imesema kuwa ugonjwa hatari wa Homa ya Nyani (Mpox) umesambaa katika kila sehemu ya taifa hilo, huku ikisisitiza wananchi kutoa...

## Utumikishaji watoto machimboni janga mimba za utotoni

UKURASA 4

**MICHEZO** FADLU, AHOUA NDIO BORA ZAIDI AGOSTI UK.24

**MAONI,** UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango (katikati), akishiriki katika Ufunguzi wa Mkutano wa 35 wa Kamati ya Kudumu ya Fedha ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unaofanyika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Marekebisho Sheria ya TAKUKURU

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2024, umependekeza kuongeza kosa na adhabu ya rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani.

Lengo la marekebisho hayo ni kuiwezesha Taasisi ya Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kufuatilia rushwa katika uchaguzi, michezo, michezo ya kubahatisha na burudani.

Hayo yalisemwa jana bungeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, wakati akiwasilisha maelezo ya muswada huo.

"Lengo la marekebisho haya ni kuiwezesha taasisi kupambana na rushwa kufanyakazi kwa ufanisi katika nyanja hizi na hivyo kuhakikisha uadilifu na haki vinadumishwa katika michakato ya uchaguzi, matukio ya michezo, shughuli za michezo ya kubahatisha na tasnia ya burudani," alisema.

Aidha, alisema adhabu ya faini isiyopungua Shilingi milioni mbili na isiyozidi Sh. milioni 10 au kifungo kisichopungua miaka mitano imewekwa kwenye makosa ya rushwa ya ngono katika Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wa mwaka 2024.

Alisema kifungu cha 25 kinaweka masharti kuwa ni kosa kwa mtu mwenye mamlaka kuomba rushwa ya ngono au kuomba upendeleo wa aina nyingine kama sharti la kutoa au kupata ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

Pia alisema kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu anayeahidi au kutoa rushwa ya ngono au upendeleo mwingine kwa mtu mwenye mamlaka au aliye katika nafasi ya mamlaka ili kumshawishi mtu huyo kutoa upendeleo wa ajira, cheo, haki au upendeleo mwingine wowote.

**USHAURI WA KAMATI**

Akisoma maoni ya Kamati ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mjumbe wa kamati hiyo, Mashimba Ndaki, alisema mapendekezo ya mabadiliko ya sheria katika kifungu cha 25 hasa ongezeko la kifungu kipya cha 25(1) (b) kimeleta hisia hasi kwa wadau waliofika mbele ya kamati, asasi za kiraia na wanaharakati mbalimbali kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

"Wadau wengi wamelalamikia kifungu hicho kwa mtazamo kuwa kinawanyima waathirika wa rushwa ya ngono haki zao stahiki na kinawapa kinga wahusika wa vitendo hivyo," alisema.

Alisema kuwa kamati ilibaini kuwa chimbuko la mapendekezo hayo ni pamoja na mikataba ya Kimataifa na Kikanda, Ibara ya 15(a) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa inaelekeza nchi wanachama kutunga Sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono, Ibara ya 4 (1) (b) ya Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa inaelekeza nchi wanachama kutunga sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

Pia, alisema Ibara ya 3 (b) ya Mkataba wa SADC dhidi ya rushwa inaelekeza nchi wanachama kutunga sheria yenye kosa la kushawishi kutoa rushwa ya ngono.

"Hapa nchini, Tanzania Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi kwenye Sheria ya 14 Kupambana na Rushwa na Makosa ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 2023 kifungu cha 52 kimeainisha kuwa ni kosa kushawishi kutoa rushwa ya ngono."

"Kamati ilijiridhisha kuwa kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, sura ya 329 imeainisha kuwa ni kosa kwa mtu yeyote ambaye atatoa au ataahidi kutoa rushwa kwa namna yoyote ile ili kupata upendeleo wowote mtu huyo atakuwa ametenda kosa la rushwa," alisema.

Hata hivyo, alisema ili kuweka mkazo kwa mtu mwenye mamlaka kutoshawishika kutoa upendeleo wa aina yoyote kwa ahadi ama kupewa rushwa ya ngono. Kamati inapendekeza kuongeza adhabu kwenye kifungu cha 25 cha sheria hiyo, kwa adhabu ya faini ukomo wa juu kutoka kuwa Shilingi milioni tano na kuwa Sh. milioni 10, na kwa adhabu ya kifungu ukomo wa juu kutoka kuwa miaka mitatu na kuwa miaka 10.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**FLAVIAN FESTO LUOGA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 799 BBE aina ya Fuso kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

Taarifa ya Polisi **PHQ/RUV/NAM/5902/2024.**

## Sheria Madini kufumuliwa kuruhusu biashara makinikia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHERIA ya Madini, Sura ya 123 imefumuliwa kupitia Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2024, na kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi ambayo awali ilikuwa imezuiliwa ili kuvutia uwekezaji katika viwanda vya madini ghafi nchini.

Akisoma maelezo ya muswada huo Bungeni jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Hamza Johari, alisema sheria hiyo ilitungwa mwaka 2010 na hadi sasa imefanyiwa marekebisho mara 13.

Alisema marekebisho yanapendekeza kurekebisha jumla ya vifungu 12 na vifungu vipya viwili vinapendekezwa kuongezwa, ibara ya 21 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha IOOD, ili kuruhusu biashara ya makinikia ndani ya nchi. Kwa sasa sheria inazuia biashara ya makinikia ndani na nje ya nchi.

Aidha, alisema Ibara ya 22 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 106 ili kuwataka wafanyabiashara wa madini walio na leseni na mawakala au madalali walio na leseni kuapa kiapo cha uadilifu na inalenga kuhakikisha utii wa sheria.

"Ibara ya 13 ya Muswada inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipya cha 271 ili kuanzisha Maabara ya Madini ya Tume ya Madini. Lengo la marekebisho hayo ni kuirasimisha taasisi hiyo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa msingi wa sheria," alisema.

Alisema Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika sheria.

Pamoja na hayo, alisema ibara ya 15 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 73 ili kutofautisha leseni za wafanyabiashara wa madini ya Tanzanite na wafanyabiashara wa madini ya vito vingine vya rangi.

"Lengo la marekebisho haya ni kuweka udhibiti wa madini ya Tanzanite kwa namna maalumu na kuyatangaza kwa kuzingatia uwapo wa madini hayo wa kipekee nchini Tanzania," alisema.

Alisema Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 86A ili kuweka masharti kwamba mwingizaji wa madini nchini hatatakiwa kulipa mirabaha kwa madini yanayoingizwa nchini endapo atathibitisha kuwa amelipa mirabaha katika nchi yalikotoka madini ili kuepusha ulipaji wa mirabaha zaidi ya mara moja.

"Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 87 kwa kuongeza viwango vya mirabaha inayopaswa kulipwa serikalini na wafanyabiashara wa madini ya vito yanayosafirishwa kwenda nje ya nchi ambayo yamenunuliwa katika minada ya madini na maonyesho ya kimataifa ya madini ya vito," alisema.

Pia, alisema Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 27 F ili kuweka adhabu kwa wamiliki wa haki za madini ambao wanatoa taarifa za uongo au zenye kupotosha au kushindwa kuwasilisha taarifa sahihi za madini.

Pia alisema Ibara ya 14 ya Muswada inapendekeza marekebisho katika kifungu cha 66 ili kuweka adhabu kwa mtu atakayeshindwa kulipa ada ya ukaguzi kama ilivyoainishwa katika sheria.

HABARI KITAIFA

# Watanzania 80% kufikiwa nishati safi

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali imejipanga hadi kufikia mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania, watakuwa wanatumia nishati safi ya kupikia nyumbani ili kuepuka ukataji wa miti unaochangia uharibifu wa mazingira.

Aidha, amesema uchafuzi wa mazingira ndani ya nyumba unaotokana na kupikia kwa kuni na mkaa ni miongoni mwa sababu kuu zinazoharibu mazingira na kuleta matatizo ya kiafya.

Dk. Mpango alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua Jukwaa la 24 na Mkutano wa 35 wa Kamati ya Kudumu ya Fedha ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC), ambao nchi ya Tanzania imekuwa mwenyeji.

Alisema Tanzania imekuwa kinara kwa bara la Afrika kwa ajenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia nyumbani (AWCCSP), kupitia Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amekuwa bingwa wa kipaumbele cha kusimamia ajenda hiyo.

Pia, lengo la kutumia teknolojia hiyo ni kuwaondolea mzigo



wanawake kutumia mkaa na kuni kupikia.

"Kwa ushirikiano na washirika wetu wa maendeleo, jumla ya Dola za Kimarekani bilioni 2.2 zilikusanywa katika Kongamano la Nishati Safi ya Kupika huko Paris, Mei 2024, haya ni maendeleo ya kutia moyo ambayo yatasaidia kukabiliana na changamoto za kimazingira, kiafya na kijamii na kiuchumi zinazohusiana na matumizi ya nishati asilia ya kupikia," alisema Dk. Mpango.

Kadhalika, serikali imejipanga ifikapo mwaka 2034, asilimia 80 ya Watanzania wanatumia nishati safi ya kupikia, kutoka asilimia saba ya sasa.

Alisema Tanzania inakabiliwa na athari kadhaa za mabadiliko ya hali ya hewa ya ukubwa usio na kifani, ikiwamo Desemba 2023, kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na kusababisha mafuriko Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara.

Watu 89 walifariki dunia, 139 walijeruhiwa, zaidi ya watu 1,500 waliathirika na nyumba 95 zikisombwa na maji.

Aidha, kulikuwa na uharibifu katika miundombinu na serikali ililazimika kuwahamisha watu na kutumia takriban Dola za Kimarekani milioni tatu kukarabati na kujenga nyumba na barabara mpya katika eneo hilo lililoathirika. Alisema uharibifu wa mtandao mzima wa barabara za kitaifa ulikuwa kilomita 520, ambazo zitahitaji Dola za Kimarekani milioni 355 kukarabati na ujenzi mpya, ustahimilivu wa hali ya hewa sasa umekuwa mojawapo ya viashiria muhimu na kanuni za msingi za ugawaji wa rasilimali za bajeti kuanzia mwaka wa fedha 2024/2025.

"Mabadiliko ya hali ya hewa na ukosefu wa usawa wa kijinsia ni changamoto, lakini Tanzania imeendelea kuhimiza ujumuishaji wa masuala ya jinsia na mabadiliko ya tabianchi katika sera, programu na mikakati katika ngazi zote kwa kuweka vipengele muhimu vya sera za usawa wa kijinsia katika upatikanaji wa fursa za kiuchumi na kifedha kwa wanawake na wanaume kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kushiriki kikamilifu katika ngazi zote za uongozi na maamuzi," alisema.

Mabadiliko ya hali ya hewa yameleta athari katika mifumo ya ikolojia, usalama wa chakula na mifumo ya afya, pamoja na kijamii, ikiwamo ya kijinsia na athari hizo kwa kiasi kikubwa zimesababisha mafuriko, ukame, kuenea kwa mimea vamizi, kuongezeka kwa usawa wa bahari na maporomoko ya ardhi ni miongoni mwa matokeo yanayoonekana zaidi ya mabadiliko ya hali ya hewa kwa bahati mbaya na kusababisha athari kwa makundi ya wanawake, vijana na watoto.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Ashati Kijaji, alisema mabadiliko ya hali ya hewa huleta hatari zinazojidhihirisha kupitia hali mbaya ya hewa, kupanda kwa joto, mvua zisizotabirika, dhoruba za kitropiki na mafuriko ambayo yameathiri uchumi na ikolojia wa jamii.

Alisema changamoto hizo husababisha hasara na uharibifu wa miundombinu muhimu, kutoka barabara na madaraja, huduma, njia za umeme kutishia huduma muhimu zinazotegemea maisha na kusababisha uhaba wa maji na upungufu chakula.

Aidha, dhoruba za kitropiki kama vile hidaya, tayari zimeharibu miundombinu ya makazi na usambazaji wa umeme, haswa katika Wilaya za Kilosa na Mvomero huko Morogoro na Zanzibar, kuna ulazima wa uhitaji wa dharura wa kuchukua hatua kabambe ya hali ya hewa ikiwamo kujenga uwezo wa kustahimili mabadiliko ya tabianchi na kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema miongoni mwa mambo mengi ni mishtuko ya mambo ya ndani na nje yanayohusu mabadiliko ya hali ya hewa katika kukabiliana na hali ya ustahimilivu.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA MARA, SIMIYU NA MANYARA (BABATI DC, HANANG DC, MBULU DC NA BABATI TC)**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na mzunguko wa nne utafanyika katika Mikoa ya Mara, Simiyu, na Manyara katika Halmashauri za Wilaya za Babati, Hanang, Mbulu na Mji wa Babati tarehe 04 hadi 10 Septemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 04 hadi Jumanne tarehe 10 Septemba, 2024.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume ***www.inec.go.tz*** au anuani ya ***ovrs.inec.go.tz*** kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 9 na kubonyeza.Kisha atachagua Namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

***KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA***
**Limetolewa tarehe 27 Agosti, 2024 na:**

Juma Rahisi.
KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**
**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya kuhuisha leseni ya kuzalisha umeme. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi dhidi ya maombi hayo. Taarifa za mwombaji, mitambo na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:-

| Na. | MAELEZO |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | *Mufindi Paper Mills Ltd.*<br>S.L.P. 01, Mufindi, Iringa. |
| **Mahali ulipo Mtambo** | Kiwanja Na. 108/1 & 108/2, Mufindi, Iringa. |
| **Taarifa za Wanahisa** | 1. *Jaswant Singh Rai*<br>S.L.P. 18309, Nairobi 00500, Kenya, **49%**<br><br>2. *Anglehurst Industries Ltd*<br>British Virgin Islands, Uingereza, **51%** |
| **Maelezo ya Mtambo** | Mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati kumi (10 MW), chanzo cha nishati kwa ajili ya Uzalishaji ni Majani |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya kuzalisha umeme kwa matumizi binafsi kwa muda wa miaka mitano (5) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu atakayewasilisha maombi kwa maandishi.

**Imetolewa na:-**
**Mkurugenzi Mkuu**

# Alalamikia sera mpya NHIF kusumbua wateja

**Na Jenifer Gilla**

MFANYABIASHARA, Shadiya Mtunzi, ameushauri Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kufanya maboresho kwenye sera mpya ya bima ya mtoto ili kuondoa sintofahamu zinazojitokeza kwa wateja wake.

Shadiya aliambia Nipashe kuwa anakosa baadhi ya huduma kwa sasa kwa kuwa mfuko huo unamtambua kama mteja mpya wakati ana zaidi ya miaka 10.

Alisema alipitia kadhia hiyo baada ya kumwingiza mtoto wake kwenye kifurushi chake na kupitia mabadiliko hayo mfuko unamtambua kama mnufaika mpya na si wa muda mrefu.

Hata hivyo, NHIF imetoa ufafanuzi na kusema kuwa utaratibu wa mwanachama anayehama kifurushi kuanza upya ni wa kawaida na unajulikana na kila mwanachama.

Kaimu Meneja Uhusiano wa NHIF, Grace Michael, alisema mwanachama anayehama kifurushi analazimika kuanza upya kwa sababu kila kifurushi kinahudumiwa na dirisha tofauti.

Awali, akitoa malalamiko hayo, Shadiya alisema alichukua uamuzi wa kumjumuisha mtoto wake katika kifurushi chake baada ya mfuko huo kuondoa kifurushi cha watoto cha kulipia 50,400 na kuwashauri wazazi wawakatie watoto wao kupitia shule au kuwaunganisha kwenye vifurushi vyao.

"Mimi ni mwanachama wa NHIF kwa zaidi ya miaka 10 nipo katika taasisi binafsi ninalipa kifurushi kikubwa kile cha timiza.

Alisema baada ya taarifa hiyo alikwenda katika ofisi zao kwa ajili ya kumwingiza mtoto wake kupitia kifurushi na kushauriwa kuwa asubiri mpaka kifurushi kiishe siku atakayokwenda kulipia upya ndipo atamwingiza mtoto wake.

Alisema siku ilipofika walimpa namba ya kulipia malipo yake na mwanawe kwa ajili ya kumwingiza katika kifurushi ambacho tayari alikuwa ni mwananchama kwa zaidi ya miaka 10.

Alisema baada ya hapo walimtengenezea kadi mpya ambayo inaonesha sio mwanachama wa zamani bali ni mpya.

Baada ya siku kadhaa, Shadya aliugua na alipokwenda hospitali kwa kutumia kadi yake akajibiwa kuwa hana sifa ya kupata huduma nyingi kwa sababu ni mwanachama mpya wakati yeye ni mwanachama wa siku nyingi.

Baada ya kupata majibu hayo alilazimika kurudi NHIF na kupewa majibu kuwa mabadiliko ya sheria ndio yaliyosababisha yote hayo, hali ilimwacha akiwa na maswali kwanini serikali ibadilishe sheria bila kujua madhara yake.

Akitoa mfano, alisema zamani alikuwa analipa Sh. 600,000 kwa mwaka akiwa peke yake sasa hivi analipia Sh. 800,000 na kwamba badala ya kuonekana wa thamani zaidi sasa anaonekana amepoteza sifa kabisa.

"Mwanachama ambaye nimekuwa ninaweka fedha zangu kila mwezi na mimi ni mfanyabiashara ninahifadhi fedha kwa ajili ya kulipia, leo baada ya miaka 10 ninakwenda kupata huduma ninaambiwa sina vigezo na mbaya zaidi hata watumishi walioko ofisini hawajui madhara yaliyopo."

"Sasa NHIF inatusaidiaje? Au inatugandamiza? Kama inaanzisha sera mpya kwa nini isifanyiwe majaribio kwanza kuona kama ni nzuri au mbaya?" Alihoji.

Shadiya alisema kwa sasa ni mgonjwa anahitaji matibabu, lakini NHIF wanataka kumtumia kama mfano akisisitiza lengo lake anataka wajue nini wanapaswa kufanya kwa ajili ya kuendeleza shirika.

Aidha, alishauri sera ibadilishwe au iangalie namna ya kumaliza changamoto hizo, akisisitiza kuwa inakandamiza mwanachama kwa sababu kumwingiza mtoto kunasababisha mtu afutiwe taarifa zake zote za nyuma.

Alisema hataki atatuliwe tatizo hilo binafsi bali anataka iwe kwa wote wanaosumbuliwa na changamoto hiyo au sera hiyo ifutwe iwe kama zamani.




Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Lihundi, akizungumza wakati wa kufunga tamasha la saba, lililofanyika kwa siku tatu la kupinga ukatili wa jinsia lililofanyika wilayani Kondoa hivi karibuni, kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya mtandao huo, Igemma Akilimali, **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Utumikishaji machimboni waongeza mimba za utotoni

**Na Mussa Mwangoka,** KATAVI

UTUMIKISHWAJI watoto na ubakaji katika maeneo ya machimbo ya madini katika Kijiji cha Dilifu, Manispaa ya Mpanda mkoani Katavi, vinatajwa kuwa chanzo cha ongezeko la mimba na ndoa za utotoni.

Pia, watoto wa kiume wanalazimishwa kuingiliwa kinyume na maumbile na kuwaathiri kifya na kisaikolojia.

Baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Dilifu, wamewaeleza waandishi wa habari wa Mkoa wa Katavi, wanaopinga vitendo vya ukatili na uharibifu wa mazingira waliotembelea maeneo hayo ya uchimbaji wa madini.

"Hii hali inasikitisha sana, watoto wadogo wa miaka 13,14 na 16 wanaingia maduarani (mashimoni) kufanya shughuli za utafutaji madini, badala ya kwenda shule.

Wengine wanafanyiwa vitendo vya ubakaji na kama ndio mabinti wanajikuta wakipata mimba katika umri mdogo hivyo kukatisha ndoto zao za kimaisha," alisema Parakisedo Limbo, mkazi wa eneo hilo.

Michael Mpangala, alisema anashangaa kuona baadhi ya wamiliki wa vitalu vya madini wakiwapokea watoto na kuwapa ajira zisizo rasmi ndani ya machimo yao, kitu ambacho ni kinyume na sheria za nchi.

Mmoja wa watoto aliyekutwa akifanya ujira ndani ya machimbo hayo, jina linahifadhiwa (16) anayesoma darasa la sita, alisema analazimika kwenda maduarani kufanya kazi za kusaidia uchimbaji kutokana na kutafuta fedha za kujikimu kimaisha.

"Mimi siwezi kwenda shule wakati sina hela ya kukidhi mahitaji yangu muhimu ikiwamo chakula, ukizingatia wazazi wangu hawana uwezo wa kiuchumi," alisema.

Mmoja wa waathirika wa kubakwa (jina linahifadhiwa) alisema alibakwa na kupewa ujauzito akiwa katika umri mdogo huku aliyembaka hajulikani halipo hadi sasa.

Ofisa Ustawi wa Jamii Wilaya ya Mpanda, Agnes Mbalaganya, alikemea vitendo hivyo na kuwataka wananchi kutoa taarifa kwa polisi matukio kama hayo yanapojitokeza.

Mkuu wa Wilaya ya Mpanda, Jamila Yusuph, alipiga marufuku watoto kutumikishwa machimboni kwa kuwa ni kinyume na sheria, huku akiahidi hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa watakaobainika kuajiri watoto katika maeneo hayo.

"Ninapiga marufuku kuanzia sasa watoto kuingia maduarani... sasa duara tutakapokuta kuna mtoto hatua kali zitachukuliwa kwa aliyemwajiri na mzazi wake," alisema.

Alikemea tabia ya watoto kutoroka shule na kwenda kwenye machimbo na maeneo mengine kwa kuwa opereshen rudisha shule inakwenda kufanyika, watakaokamatwa watarejeshwa shuleni.

Ripoti ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria Tanzania ya mwaka 2022 inautaja Mkoa wa Katavi kuwa wa tatu kwa mimba na ndoa za utotoni ukiwa na asilimia 34, ukiongozwa na Songwe asilimia 45, Ruvuma asilimia 37.


**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**SOPHIA SAIDI NAMOYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji yenye namba za usajili **MC372BBK.** Chasis namba **MD2AA24ZZRWF24871** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/185589/2024**



**KUPOTEA KWA CHETI**



**ROZIANA SIMON PETER** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0207-0092** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIRAENI GIRSL SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/187175/2024.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa DSM**

**Shauri la madai/Ndoa Na. 205/2024**

**Jina la mdai AGGREGATE CRUSHING IND LTD**

**Jina la mdaiwa JOYCE B. MMASI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika mahakama za mwanzo)**

**Kwa JOYCE B. MMASI**

**Kwa kuwa mdai/ wadai ameleta/ wameleta madai yako/yao kwamba (eleza hapa habari za madai)**
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 13 mwezi 9 mwaka 24 saa 7:00 mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 mwezi 8 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**

**Kituo cha MAKOLE Mkoa Dodoma**

**Shauri la Madai/Ndoa Na 73/2024**

**Jina Mdai EUTICHIUS EMMANUEL NSHUNJU**

**Jina la Mdaiwa BERNARD MSONSAH**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**( Kanuni ya 18 ya kanuni za Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa BERNARD MSONSAH**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta madai yake /yao kwamba**
**(Eleza hapa habari za Madai )**
**MADAI YA TSH 5,000,000/=(MILIONI TANO)**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 6 Mwezi 9 Mwaka 2024 saa 2:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 2 Mwezi 9 Mwaka 2024



**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**Probate and Administration Cause No 21429 Of 2024**

**In the matter of the estate of the late JOYCE NICOLAUS LUSAMBO of Msembeta within Dodoma City**

**And**

**In the matter of application for letters of administration by JOSEPH NICHOLAUS LUSAMBO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN NO. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on before the 2 day of 10.........................2024
Dated at Dodoma this 2 day of 9................ 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

# Kigezo cha umri katika ajira chazua mjadala bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KIGEZO cha umri usiozidi miaka 25 katika ajira za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), zilizotangazwa hivi karibuni kimeibuliwa bungeni huku wabunge wakiishauri serikali kuondoa na kuangalia namna ya kuweka vigezo vitakavyoruhusu vijana wengi kuchangamkia fursa hiyo.

Agosti 31, 2024 taasisi hiyo ilitoa tangazo la nafasi za kazi 351 kupitia tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Suala hilo liliibuliwa bungeni na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ngw'asi Kamani ambaye aliomba Bunge kujadili hoja ya dharura na kubainisha kuwa kati ya vigezo vya waombaji kwenye nafasi hizo ni umri usiozidi miaka 25.

"Kwa elimu yetu ya kawaida mwanafunzi anamaliza elimu ya kidato cha nne akiwa na miaka 18 na akimaliza kidato cha sita 21 na akiingia chuoni anakwenda hadi miaka 24, lakini nafasi hizi umri usiozidi miaka 25, nafasi hizi ni chache na waombaji ni wengi ikiwezekana umri uongezwe ili vijana waliopo mtaani wanufaike," alisema.

Alisema ni vyema umri uongezwe hadi miaka 30, ili kutoa fursa kwa vijana wengi kuomba na wasihukumiwe kwa umri.

Akifafanua hoja yake, Mbunge Kamani alisema kila mwaka wanaohitimu vyuo ni kuanzia 100,000 hadi 300,000 na nafasi za kazi ni chache.

Kutokana na hoja hiyo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alimpa nafasi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala, George Simbachawene, ambaye alisema katika umri huo ni kigezo cha majeshi ili wanaochukuliwa wawe na ukakamavu.

"Tunafahamu kwamba nafasi zilizotangazwa sio za wahitimu tu, hawa tunahitaji ambao wataenda kupewa mafunzo porini na ndio maana wanachukua watu wenye umri usiozidi miaka 25, kwa sheria yetu ya utumishi wa umma ni umri usiozidi miaka 45 hivyo tukichukua wa miaka 45 hakika hataweza mafunzo haya ya kijeshi," alisema.

Waziri Simbachawene alisema tangazo linawahitaji wa kada za kawaida na kwamba lazima wapite mafunzo ya kijeshi na umri huo ni kigezo cha kupima ukakamavu.

Aliahidi serikali itachukua maoni ya wabunge na kuyafanyia kazi.

Hata hivyo, kutokana na majibu hayo Spika Tulia alitoa fursa kwa wabunge kujadili ili kuishauri serikali.

"Jambo hili si mara ya kwanza kujitokeza bungeni kuhusu vigezo vya ajira, maeneo ya jeshi na jeshi usu na tulisema kwasababu ya jeshi wana vigezo vya ziada, lakini tulishashauri na kwa kuwa linakwenda na kurudi ni vyema serikali ipate ushauri," alisema Spika.

**WALICHOSEMA WABUNGE**

Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Saputu, alisema suala la umri hata kama ni jeshi usu ni vyema wataalamu wakatafakari hali za Watanzania na vijana waliopo mtaani kwa kukosa ajira.

"Hiki kigezo cha umri hakipo sawa kwasababu Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na jeshi usu mafunzo hayawezi kufanana, suala la umri liwe hadi miaka 30, suala la afya likajulikane kwenye mafunzo huko baada ya kupimwa, kuweka miaka 25 ni kuwazuia vijana wengi kupata ajira," alisema.

Mbunge wa Tarime Vijijini (CCM), Mwita Waitara, alisema umri uongezwe watu waombe kama ni suala la mazoezi mtu ashindwe mwenyewe.

Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Sophia Mwakagenda, alisema kuweka umri wa miaka 25 kutawaweka vijana wengine nje, kwa kuwa ni muda mrefu ajira hazijatoka.

**KAULI YA SPIKA**

Baada ya maoni ya wabunge, Spika Tulia alisema; "Nakumbuka tulisema kwa upande wa jeshi kwasababu wana vigezo vya ziada waache hivyo na hizi taasisi nyingine ziangalie ambazo hazihitaji hiki kigezo cha watu kupitia mafunzo hayo.

Alisema kwa kuwa Mbunge mwenye hoja hajatoa azimio la kuazimiwa na Bunge, serikali ichukue ushauri wa wabunge kwa yale yanayoweza kurekebishika yarekebishwe.

"Kwa mfano haya ya dereva wa JWTZ hawezi kulingana na wa TAWA, ukitaka kuweka vigezo sawa ni bora tuwapeleke wote sasa wakapate mafunzo ya jeshi halafu watawanywe kwenye majeshi," alisema.

Alisema serikali ione utofauti ili isiwaondoe kwenye mfumo wa ajira na kwamba kuna mambo yanazungumzika na waweke mazingira kuwa kwa aina ya mafunzo ambayo mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka 25 anaweza, apewe fursa.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TARURA, Watanzania wanatarajia makubwa kwenye barabara vijijini

**WAKALA** wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imetangaza mafanikio ya mipango mikakati yake iliyojiwekea kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2021 kwa asilimia 50.

Mikakati hiyo ni pamoja na kuboresha baadhi ya barabara na madaraja katika wilaya mbalimbali nchini.

Lengo la TARURA ni kuhakikisha inarahisisha mawasiliano ya barabara nchini kwa wananchi kufuata huduma maeneo ya mijini, wafanyabiashara kusafirisha bidhaa zao kutoka sehemu moja kwenda nyingine kwa kutumia magari.

Kwa upande mwingine ni wakulima mazao ya chakula kutoka mashambani hususani maeneo ya vijijini hadi mjini kusaka masoko na kukuza uchumi wao kwa kujiingizia kipato.

TARURA wanahitaji pongezi kwa kufanikisha mpango mkakati huo kwa asilimia 50 kati ya asilimia 60 ambazo wamejiwekea kwa kipindi hicho.

Kiwango hicho ambacho TARURA wamefikia si kidogo kwa watu wanaopenda maendeleo bali ni kikubwa kulingana na changamoto ambazo wamekuwa wakikabiliana nazo wakati wa utekelezaji mipango mikakati hiyo ili kuondoa kero kukosekana kwa usafiri kutokana na maeneo yao kutofikika kwa ubovu wa barabara na ukosefu wa madaraja.

Pamoja na maeneo mengi ya mijini kukabiliwa na changamoto za kuwa na barabara nyingi za mitaa kuwa mbovu na nyingine kugeuka mashimo kwa kumegwa na mafuriko ya mvua kwa kukosa mitaro, jitihada zaidi zinapaswa kuelekezwa vijijini.

Tunashauri jitihada hizo zielekezwe vijijini kwa sababu kuna idadi kubwa ya wakulima ambao wanategemewa kwa kulisha idadi kubwa ya Watanzania wanaoishi mijini kutokana na mazao wanayolima.

Sio siri, wakulima kila mwaka wamekuwa wakilalamika kupata hasara kutokana na mazao yao kuharibika kwa kukosa usafiri wa uhakika hasa wakati mvua zinaponyesha kwa ubovu wa barabara wa kusafirisha mazao yao hadi mijini kwa ajili ya kuwauzia walaji.

Hivyo, ili kufanikisha hilo, TARURA inapaswa kutekeleza jukumu lake kama ilivyoelekezwa na Mtendaji wake mkuu, Victor Seff kwa kuzipandisha hadhi barabara za wilaya hususani za vijijini kutoka kiwango cha udongo kuwa za changarawe na hata za changarawe kuwa za lami.

Kwa kufanya hivyo, hatua hiyo ndio itakuwa mwarobaini wa kukabiliana na tatizo la kuharibika na kutoweka kwa barabara badala ya kuishia kuzikarabati tu kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa baadhi ya barabara kuu na za mitaa kwa maeneo husika.

Kikubwa cha kuzingatia ni kuweka mifereji ya kupitishia maji kwenye barabara hizo ili ziweze kudumu kwa muda mrefu kuepusha maji hayo kutuama kwenye barabara hizo na kuleta uharibifu.

Miundombinu ya barabara ndio mkombozi mkubwa wa maendeleo hasa katika sekta ya usafirishaji.

Barabara hizo zinapaswa kujengwa na kukarabatiwa kwa namna ambayo wataalamu wanaona inafaa ili kuhakikisha zinadumu kwa muda mrefu kwani hatua hiyo itachochea maendeleo na uchumi kwa wakulima, wafanyabiashara na wananchi wengine wa kawaida na serikali kupata mapato kutokana na kukusanya kodi.

Vilevile ifanye hivyo kwa kujenga madaraja kwa kiwango cha ubora unaotakiwa ili kuhakikisha mawasiliano ya barabara kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kwa vyombo vya usafiri kuvuka.

Sababu mbalimbali, ikiwamo ufinyu wa bajeti inayotolewa na Serikali kwa Ofisi ya Rais Tawala za Serikali (TAMISEMI) kwa ajili ya TARURA, isiwe kikwazo kwani kauli hizo ni suala mtambuka tu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Tuache visingizio, tuwapatie chakula wanafunzi shuleni

Na Sabato Kasika

**WIZARA** ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inahimiza kuwapo kwa chakula shuleni, lakini wazazi na walezi lazima washiriki kuwalisha watoto.

Aidha, wizara inaeleza kuwa ili kupata matokeo bora darasani na kwenye elimu, ni lazima wanafunzi wapate chakula shuleni. Mwili wenye njaa hauwezi kuwa na ubongo unaofanyakazi.

Inahimiza chakula bora, kwa kuwa ndicho ambacho kinaweza kuwajengea wanafunzi afya bora na kupata utulivu wa akili wawapo madarasani wakiendelea na vipindi vya masomo.

Ni kauli ya Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ambayo ameitoa, katika moja ya hotuba zake, huku akisisitiza kupatikana kwa huduma ya chakula shuleni.

Lakini, anagusia kuwa huduma ya chakula na lishe shuleni ni suala mtambuka linalohitaji ushiriki wa sekta na wadau mbalimbali, kwa ajili ya kusaidia kupata matokeo chanya.

Pamoja na umuhimu wa chakula shuleni, bado kuna changamoto kadhaa, ambazo zinakwamisha baadhi ya shule kutokuwa na huduma hiyo na kusababisha baadhi ya wanafunzi kushinda njaa.

Miongoni mwa changamoto hizo, ni baadhi ya wazazi na walezi kutokuwa tayari kuchangia chakula hicho, kwa maelezo kuwa serikali ilishatangaza kuwa elimu ni bure.

Kwa kuwa serikali ilishatangaza kutoa elimu bure, wanaamini kwamba hata suala la chakula, inatakiwa kugharimia, kitendo ambacho ni wazi kinaweza kukwamisha mpango wa kutoa huduma hiyo shuleni.

Hivyo, licha ya serikali na baadhi ya wadau kujitahidi bado wapo wanafunzi wasiopata huduma hiyo, kutokana na sababu ambazo ninaamini ziko ndani ya uwezo wa wazazi na walezi.

Ninadhani kuna haja kwa wazazi na walezi wenye msimamo huo, kubadilika na kutambua utoaji wa chakula shuleni ni kwa manufaa ya watoto wao, hivyo, wasiendelee kung'ang'ania jambo lisilo na tija.

Suala la chakula shuleni ni la wazi, kwani limewekewa mwongozo, hivyo, ni wazi wazazi na jamii imeshirikishwa juu ya mpango huo ili wawe sehemu au wamiliki wake katika utolewaji wa chakula.

Haihitaji kuelekezwa au kuelimishwa kwa muda mrefu kutambua umuhimu wa chakula shuleni, kwani sidhani kama kuna mtu asiyejua umuhimu wa kupata chakula awe shuleni au nyumbani.

Wapo ambao husema wanataka kuelimishwa kwa kina juu ya faida ya kuwapatia wanafunzi chakula shuleni ili waelewe. Huo unaweza kuwa ujanja wa kutaka kukwepa majukumu.

Labda jambo ambalo wangelikazania, ni kuhimiza uwazi kwenye michango ya fedha ambayo wanaitoa kwa ajili ya chakula au chakula wanachokitoa kwani eneo hilo ni miongoni mwa yale yanayolalamikiwa.

Mbali na hilo, eneo lingine linalolalamikiwa ni kwenye usimamizi wa fedha na uhifadhi wa vyakula kwani fedha zinahitaji usimamizi mzuri ili ziendane na bajeti iliyopangwa.

Hivyo, wazazi na walezi wangeng'ang'ana ili maeneo hayo yawe wazi, kwani kukosekana kwa uwazi kunaweza kusababisha watu kuhisi kuwa michango yao inatumiwa vibaya na walimu.

Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa naye amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuendelea kusimamia kikamilifu fedha zote zinazopangwa za kutekeleza afua za lishe shuleni.

Kwa maelekezo hayo, hata walimu, kamati na bodi za shule ni muhimu kutengeneza mazingira ambayo yatawashawishi wazazi na walezi kutoa fedha au chakula kwa ajili ya chakula cha watoto wao.

Ninaamini hatua hiyo inaweza kuwajengea uaminifu kwa jamii na kuwafanya wazazi na walezi watoe fedha zao bila kusukumwa, lakini hatua hiyo itapunguza visingizio vya baadhi ya wazazi na walezi ambao hujiweka pembeni wakidhani hawahusiki kuchangia chakula shuleni.

HABARI KITAIFA

## CTI na Tantrade kukutanisha viwanda 500 Dar

**Na Joseph Mwendapole**

SHIRIKISHO la Viwanda Tanzania (CTI), kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), wameandaa maonesho ya kimataifa ya wenye viwanda (TIMEXPO 2024) yatakayoshirikisha viwanda 500.

Mkurugenzi Mkuu wa CTI, Mhandisi Leodegar Tenga, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa maonesho hayo yatafanyika Septemba 26 hadi Oktoba 2, katika Viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam.

Waoneshaji 500, wanatarajiwa kuonesha bidhaa mbalimbali pamoja na huduma za viwanda.

Kaulimbiu ya maonesho ya mwaka huu ni; 'Tunajenga Daraja: Kuunganisha Wazalishajii wa Ndani na Nje ya Nchi' na kwamba TIMEXPO 2024 inalenga kuonesha maendeleo katika sekta mbalimbali hususani ya viwanda.

Alisema kwa ushiriki wa zaidi ya waoneshaji 200 wa kimataifa, ni ongezeko la shauku ya kimataifa katika soko la Tanzania na fursa zinazotolewa.

Alisema washiriki hao wataonesha utaalamu wao na bidhaa za ubunifu, hivyo kuwezesha viwanda vya Tanzania kupata teknolojia mpya na kuanzisha mahusiano ya kimkakati.

"Ushiriki wa waoneshaji zaidi ya 500 katika TIMEXPO 2024 unaonesha sifa zinazoongezeka za tukio hili kama jukwaa kuu la ubunifu wa viwanda. Tuna hamu ya kuwezesha kubadilishana mawazo, teknolojia, na utaalamu ambao mchanganyiko huu wa waoneshaji wa kimataifa na wa ndani utaleta," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Uhamasishaji Biashara wa Tantrade, Tito Nombo, alisema TIMEXPO 2024 itatoa fursa ya kipekee kwa washiriki kuangalia mwenendo wa sekta ya uzalishaji kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali ili kugundua changamoto na kupata suluhisho ambalo linaweza kuongeza maendeleo ya sekta hii ya uzalishaji.

Alisema tukio hilo litahusisha sekta mbalimbali, ikiwa ni pamoja na vifaa vya ujenzi, utengenezaji wa vifaa vya uzalishaji, usindikaji wa kilimo, nguo, dawa, teknolojia za nishati mbadala na nyingine nyingi.

# Kundi la tembo lavamia shamba na kuua mkulima

**Na Stevie Chindiye,**
TUNDURU

MKAZI wa Kijiji cha Nyerere wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma, Yusuf Pole (57), auawa kwa kukanyagwa na tembo.

Mashuhuda wa tukio hilo wamesema kuwa Pole alikutwa na mkasa huo akiwa shambani kwake katika eneo la mashamba ya Namatuli Kati, katika Kata ya Mtina baada ya kundi la tembo kumvamia, kumkanyaga na kusababisha kifo chake.

Shuhuda wa tukio hilo, Mawazo Katuyo, alisema lilitokea majira ya saa tisa alasiri Agosti 31 na mwili wa marehemu ulikutwa ukiwa umeharibika huku mguu wake wa kulia ukiwa mbali na kiwiliwili chake.

Alisema eneo la tukio lilikuwa limevurugika na mtu huyo alikanyagwa maeneo ya tumboni na kusababisha baadhi ya viungo vya ndani ukiwamo utumbo kutoka nje.

Diwani wa Kata ya Mtina, Omari Majoja, alithibitisha kuwapo kwa tukio hilo na kueleza kuwa Pole alikuwa mkazi wa Kijiji cha Nyerere.

Mtendaji wa Kijiji cha Nyerere, Hadija Lukanga, alisema mwili wa marehemu uliamuliwa ubaki katika eneo la tukio kwa ajili ya taratibu za kisheria.

Pia alisema tukio hilo waliliripoti polisi na Idara ya Wanyamapori.

Kaimu Ofisa Wanyamapori wa Wilaya ya Tunduru, Ruvuma, Dunia Almasi, alisema ameshapeleka askari wa idara hiyo wenye silaha kwa ajili ya kuwafukuza tembo hao ili wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.

Alisema takwimu kutoka katika ofisi yake zinaonesha kuwa hilo ni tukio la 14 la watu kuuawa na tembo kwa kipindi cha kuanzia Januari hadi Agosti, mwaka huu.

Aidha, ofisi yake kwa kushirikiana na wadau wa uhifadhi hutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa wananchi kujikinga na matukio ya wanyama wakali na waharibifu wa mazao wakiwamo tembo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, akizungumza na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Hisa Dar es Salaam (DSE), Peter Nalitolela (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Miradi wa Soko hilo, Benjamin Abdallah na Meneja Maendeleo na Biashara wa soko hilo walipokutana bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Zaidi ya wananchi 156 Moro wapata msaada kisheria

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WANANCHI 156 wa Manispaa ya Morogoro wamepata msaada kutoka shirika linalotoa huduma za msaada wa kisheria (MPLC) baada ya kuanzisha jukwaa la jamii, wengi wao wakiwa na changamoto za migogoro ya ukatili wa kijinsia, kifamilia ikiwamo mirathi na ndoa, migogoro ya ardhi na matunzo ya watoto.

Mkurugenzi wa MPLC, Amani Mwaipaja, alisema hayo jana wakati wa jukwaa la tatu la jamii lililofanyika mjini hapa kuwa watu wanafanyiwa ukatili bila wao wenyewe kujua kutokana na kutojua sheria na kwamba kwa fursa hiyo wamehudumia watu wengi kwa wakati mmoja.

"Wapo watu wengi ambao wao huingia kwenye mahusiano wanawazalisha watoto wa kike halafu wanakimbia matunzo na kusababisha migogoro ya kifamilia, hivyo kuna migogoro ya mmoja mmoja na makundi ya watu ambayo inakosa utatuzi kwa watu kutojua sheria," alisema.

Mwaipaja alisema wananchi zaidi ya 600 wameshapata elimu kupitia mada zilizotolewa na asasi mbalimbali za kiserikali na zisizo za kiserikali ikiwamo mitazamo ya kisheria na elimu za mambo mbalimbali ya kijamii iliyotolewa kwenye jukwaa hilo.

Aidha, Mwaipaja alisema jamii inapaswa kushiriki majukwaa hayo yanayofanyika mara moja kila mwezi ili kupata elimu bila kusubiri kupata tatizo na kwenda kupewa elimu ya kisheria na msaada kwenye ofisi za MPLC.

Alisema shirika hilo linaendesha programu hiyo kwa kuifikia jamii kwa lengo la kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan katika kutoa huduma ya msaada wa kisheria anayoiendesha kwa sasa.

Mwakilishi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayojihusisha na masuala ya kupingana na umaskini (ICO), Witness Foya, alisema katika jamii hukumbana na changamoto za umaskini zinazofungamana na masuala ya kisheria.

Alisema mara kadhaa wanapokea watu waliojisusa na kuacha kujisaidia licha ya kuwa na mali isiyokuwa mkononi mwao kutokana kukabiliwa na umaskini wa kipato na umaskini wa kutojua sheria na wao humsaidia aliyedhurumiwa na kumpeleka kwenye vyombo vya kisheria ili asaidiwe na kupata haki yake.

Aliitaka jamii kufika kenye majukwaa hayo wanayosaidia kisaikolojia, kisheria, kiafya, elimu ya ujasiriamali na kuikwamua jamii kutoka walikojisusa ambao kufika kwao kutasaidia kujifunza na kujikwamua kwenye umaskini.

Mkazi wa Misufini Manispaa ya Morogoro, Boniface James, aliishukuru MPLC kwa kuanzisha jukwaa hilo ambalo limemsaidia kupata elimu na kutambua kuwa, jamii inaweza kupata misaada ya kisheria bure huku ikiwa na haki ya kusikilizwa kutokana na kuwapo kwa baadhi ya mashirika yanayosaidia watu na kujitolea katika masuala mbalimbali ya kijamii.

TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

# MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | GBP – TSN Oil Pipeline, S.L.P 12288, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "T", Eneo la Kisosora, Chumbageni, Tanga. | Ahmed Mohamed Baghazah (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Bomba la Kupokelea Mafuta |
| 2. | Nasra Khalid Shaffi, S.L.P 381, Handeni. | Kiwanja Na. 707 & 709, Eneo la Kange, Tanga. | Nasra Khalid Shaffi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 3. | Rahisi Petroleum Limited, S.L.P 7610, Moshi. | Kijiji cha Roo, Shamba Na. 1267/2/, Hai, Kilimanjaro. | Thomas Philemon Ndesamburo (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 4. | Kija Dotto Ng'hwani, S. L. P 73, Kishapu – Shinyanga. | Kiwanja Na. 177, Kitalu "A", Eneo la Itinje, Meatu, Simiyu. | Kija Dotto Ng'hwani (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 5. | Punguja Luhumbika Majani, S. L. P 09, Sengerema. | Kijiji cha Kahunda, Buchosa, Mwanza. | Punguja Luhumbika Majani, (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 6. | Adri Energies, S. L. P 2901, Dodoma. | Kiwanja Na. 62, Kitalu "GG", Eneo la Buhare, Musoma. | Alpha Pastory Mangula (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 7. | Gyunda General Supply, S. L. P 30, Ngara. | Kijiji cha Mukikomero, Ngara, Kagera. | Deogratius Nicholaus Kidenke (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta. |
| 8. | Washa Investment, S.L.P 2, Namanyere - Nkasi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Isunta - Namanyere, Nkasi, Rukwa. | Washa Luponya Udodi (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 9. | Donasian Cornel Mkusu, S.L.P 67315, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 171, Eneo la Kwembe, Ilala, Dar es Salaam. | Donasian Cornel Mkusu (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 10. | Admire Oil Ltd, S.L.P 7494, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P20810, Eneo la Toangoma, Temeke, Dar es Salaam. | Said Mire Artan (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 11. | Salmo Oil Limited, S.L.P 732, Kigoma. | Kiwanja Na. 5, Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Mohamed Nassor Ally (Mtanzania) | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Maganzo (Mfs) Energy, S.L.P 68217, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 129, Kitalu "VV", Eneo la Limele, Bagamoyo, Pwani. | Charels Pius Tungu (Mtanzania) | Kibali cha ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 13. | Juma Yusufu Kishari - Piho Petrol Station, S.L.P 830, Chemba, Dodoma. | Kiwanja Na. CDC/PH/SRR/01, Eneo la Piho, Chemba, Dodoma. | Juma Yusufu Kishari (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 14. | Mohamedi Hussein Mohamedi T/A Makuyu Filling Station, S.L.P 103, Kibaya. | Kijiji cha Makuyu, Gairo, Morogoro. | Mohamedi Hussein Mohamedi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 15. | Govidet Negelo (T) Limited, S.L.P 40556, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "E", Mvomero, Morogoro. | Selestine Benedict Mhagama (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 16. | Majaliwa Sagumo Chitembele T/A Mc Energy, S.L.P 73, Gairo. | Kijiji cha Kichangani, Gairo, Morogoro. | Majaliwa Sagumo Chitembele (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 17. | Neema Oil - Malinyi Petrol Station, S.L.P 18, Malinyi. | Kiwanja Na. 85, Ulanga, Morogoro. | Mabirika James Mabirika (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 18. | Lake Oil Gairo, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "Q", Gairo, Morogoro. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 19. | Fab International Ltd – Ikungi, S.L.P 70419, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Ikungi, Singida. | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 20. | Fab International Ltd – Rungwa, S.L.P 70419, Dar es Salaam. | Kijiji cha Rungwa, Manyoni, Singida. | Farid Ahmed Bazar (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 21. | Infinity Oil Co. Ltd - Manyoni Petrol Station, S.L.P 1280, Mbeya. | Kiwanja Na. 563, Kitalu "MM", Eneo la Majengo, Manyoni, Singida. | Said Mohamed Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 22. | Lyawere Company Limited, S.L.P 6290, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A" Eneo la Isaka, Kahama, Shinyanga. | Gasper Ezron Tesha (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 23. | Omegera Company Limited - Kizumbi Petrol Station, S.L.P 1084, Shinyanga. | Kiwanja Na. 47, Kitalu "A" Eneo la Nhelegani -Service Industry, Shinyanga. | George Marwa Migera (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 24. | GBP (T) Ltd - Tabora Road Service Station, S. L. P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 7N, Kitalu "E", Eneo la Nyamwezi, Nzega, Tabora. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 25. | Ally Mohamed Salim T/A Uroil Petrol Station, S. L. P 185, Urambo. | Kiwanja Na. 25, Kitalu "R", Eneo la Urambo, Tabora. | Ally Mohamed Salim (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 26. | Mount Meru Petroleum Limited - Kigwa, S.L.P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 2, Kitalu "A" Eneo la Matanda, Uyui, Tabora. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta. |
| 27. | Salmo Oil Limited - Kazuramimba, S.L.P 732, Kigoma. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A" Eneo la Kazuramimba, Uvinza, Kigoma. | Mohamed Nassor Ally (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 28. | Abdallah Ally Soud T/A Esso Service Station, S. L. P 119, Mpanda. | Kiwanja Na. 9, Kitalu "F", Eneo la Misunkumilo, Mpanda, Katavi. | Abdallah Ally Soud (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 29. | Lake Oil Limited, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 99/1, Kitalu "D", Eneo la Bombambili, Geita. | Ally Edha Awadh (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 30. | NGS Petroleum Limited, S.L.P 20, Bariadi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "S", Eneo la Mbugani, Geita. | Njalu Daudi Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 31. | Tabasam General Merchants Limited, S.L.P 83, Sengerema. | Kiwanja Na. 18, Block "A", Eneo la Kasamwa, Geita. | Hamis Hussein Mwagao (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 32. | GBP Tanzania Limited, S.L.P 6185, Mwanza. | Kiwanja Na.219, Kitalu "D", Eneo la Nyankumbu, Geita. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 33. | Ochele Service Station Company Limited, S.L.P 250, Rorya. | Kijiji cha Kigangama, Magu, Mwanza. | Charles Ochele Obuto (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 34. | GBP Tanzania Limited – Nyakato Service Station, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 86, Kitalu "F", Eneo la Viwanda Nyakato, Mwanza. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 35. | Blue Wave Emporium Limited, S.L.P 11624, Mwanza. | Kiwanja Na.236, Kitalu "A", Eneo la Wita Kisesa, Magu, Mwanza | Ephrahim Stanley Fimbo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 36. | Bustemma Universal Traders Limited, S.L.P 32604, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 220, Kitalu "E", Eneo la Buhongwa, Nyamagana, Mwanza. | Steven Mhele Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 37. | Magen Agro and Construction Company, S.L.P 46, Mwanza. | Kijiji cha Nkalalo, Kwimba, Mwanza. | Kasalali Emmanuel Mageni (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 38. | Nsagali Petroleum Products (T) Limited, S.L.P 20, Bariadi. | Kiwanja Na. 3 & 4, Eneo la Viwanda, Bariadi, Simiyu. | Emmanuel Gungu Silanga (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 39. | Mwita Mnaka Ohura, S.L.P 219, Bunda. | Kiwanja Na. 143, Kitalu "A", Bunda, Mara. | Mwita Mnaka Ohura (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 40. | Rashid Mashaka Rashid, S. L. P 98, Kilindi. | Kijiji cha Negero, Kilindi, Tanga. | Rashid Mashaka Rashid (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 41. | Rashid Hemed Mashaka – Kibirashi Petrol Station, S.L.P 78, Kilindi. | Kijiji cha Kibirashi, Kilindi, Tanga. | Rashid Mashaka Rashid (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 42. | Jabir Abdi Patwa T/A Usambara Filling Station, S. L. P 54, Mombo -Tanga. | Kiwanja Na. 2/13 & 2/14, Kitalu "A", Eneo la Mombo, Korogwe, Tanga. | Jabir Abdi Patwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 43. | GBP Tanzania Limited – City Service Station, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 518, Kitalu "Z", Eneo la Usagara, Tanga. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 44. | Oryx Energies Tanzania Limited, S.L.P 9540, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 62, Eneo la Viwandani, Korogwe, Tanga. | Kalpesh Kantilal Mehta (Raia wa Uingereza) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

# TANGAZO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 45. | Mount Meru Petroleum Limited - Meru 5, S.L.P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "S", Barabara ya Sokoine, Eneo la Majengo, Arusha. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 46. | Mount Meru Petroleum Limited - Mirerani Petrol Station, S.L.P 7094, Arusha. | Kiwanja Na. 2725, Eneo la Naisinyai, Simanjiro, Manyara. | Atul Mittal (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 47. | Chipukizi Tanzania Investment Co. Ltd, S.L.P 2589, Mbeya | Kiwanja Na. 4, Kitalu "O", Mbeya. | Anitha Njelela Mwakyoma (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 48. | KBG Logistics Co. Limited, S.L.P 4604, Mbeya. | Kijiji cha Itamboleo, Mbarali, Mbeya. | Keneth Beny Goliama (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 49. | VIVO Energy Tanzania Limited, S.L.P 78470, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 149, Kitalu "H", Makambako, Njombe. | Emmanuel Singilimo (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 50. | Shiuya Company Limited, S.L.P 66, Mbozi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "B", Mahenje Mbozi, Songwe. | William Yamwetela Mwashiuya (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 51. | Central Africa Energy Limited, S.L.P 5297, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 3, Eneo la Viwandani, Mbinga, Ruvuma. | Mehboob Osman (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 52. | Salam Petroleum Limited, S.L.P 100049, Dar es Salaam. . | Eneo la Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Abdirahman Mohamed Musa (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 53. | Delina Oil & Gas Distributors Limited, S.L.P 16351, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 19, Kitalu "A", Eneo la Sinza, Ubungo, Dar es Salaam. | Yuda Peniel Mosha (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 54. | Gulled Marketlink Limited, S.L.P 55038, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "167", Eneo la Ubungo Kisiwani, Ubungo, Dar es Salaam. | Adan Abdi Musa (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 55. | Swiftline Oil Limited, S.L.P 100049, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 8, Eneo la Kariakoo, Ilala, Dar es Salaam. | Mukhtar Abshir Deria (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 56. | AZMI Energy Limited, S.L.P 3476, Dar es Salaam. | Jengo la City Mall, Ilala, Dar es Salaam. | Said Abdiaziz Warsame (Raia wa kenya) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 57. | Mogas Tanzania Limited, S.L.P 70284 Dar es Salaam | Kiwanja Na. 310/3, Eneo la Kurasini, Temeke Dar es Salaam. | Geofrey Rugazoora (Raia wa Uganda) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 58. | Oilcom Tanzania Ltd, S.L.P 20831, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 4. 312 & 355, Eneo la Mandela Road, Kurasini, Temeke, Dar es Salaam. | Ameir Munif Abdallah Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Mafuta |
| 59. | Oilcom Tanzania Ltd, S.L.P 20831, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 311, Eneo la Kurasini, Temeke, Dar es Salaam. | Ameir Munif Abdallah Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Jumla ya Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 60. | Africa Fuels and Lubricants Limited, S.L.P 40063, Dar es Salaam | Kiwanja Na. 20, Kitalu "20", Nyerere Road - Chang,ombe, Ilala, Dar es Salaam. | Harish Kumar Raju (Raia wa India) | Leseni ya Jumla ya Vilainishi |
| 61. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Eneo la Buguruni, Barabara ya Mandela, Ilala, Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 62. | Oilcom (T) Ltd - Mikocheni, S.L.P 20831, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 89, Barabara ya Ally Hassan Mwinyi, Kinondoni, Dar es Salaam. | Ameir Munif Abdallah Nahdi. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 63. | Uno Petroleum Limited - Kisewe, S.L.P 2860, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 2003, Kitalu "A", Eneo la Kisewe Chamazi, Temeke, Dar es Salaam. | Diwakar Dubey. (Raia wa ndia) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 64. | Afroil Investment Limited, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. P28455, Eneo la Kwembe, Ubungo, Dar es Salaam. | Hilmy Ahmed Mbarak (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 65. | Giraffe Oil Company Ltd - Madale Petrol Station, S.L.P 79052, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 24, Kitalu "B", Eneo la Madale, Kinondoni, Dar es Salaam. | Caroline Fidelis Owenya. (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 66. | Puma Kigamboni Dege Service Station, S.L.P 9043, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "M", Eneo la Kigamboni Dege, Kigamboni, Dar es Salaam. | Fatma Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 67. | Africa Energy Ltd S.L.P 22786 Dar Es Salaam | Kiwanja Na. 6, Kitalu "L", Eneo la Mbezi Service Trade Area, Kinondoni, Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 68. | Gapco Tanzania Limited, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 80, Eneo la Mbagala, Temeke, Dar es Salaam. | Mamadou Ngom (Raia wa Senegal) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 69. | Excel Energies, S.L.P 25502, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 20, 21, 22, 23 & 30 Kitalu "E", Ilala, Dar es Salaam. | Emmanuel Azzory Marwa (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 70. | GBP Tanzania Limited - Mjimwema, S.L.P 3728, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 69, Kitalu "2", Eneo la Kisota, Kigamboni, Dar es Salaam. | Badar Seif Sood (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 71. | Darpco Energy Co. Ltd - Mbagala Charambe, S.L.P 3892, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 597, Kitalu "DD", Mbagala Charambe. Temeke Dar es Salaam. | Thabit George Mkassi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 72. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 6, Kitalu "L", Eneo la Mbezi, Kinondoni. Dar es Salaam. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 73. | M&P Exploration Production (T) Ltd S.L.P 80460, Mtwara. | Eneo la Mdimba, Mtwara. | Nicolas Engel (Raia wa Ufaransa) | Leseni ya Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 74. | Mtwara Bulk Storage Terminal Ltd, S.L.P 1419, Mtwara. | Kiwanja Na. 1, Barabara ya Bandari, Mtwara | Leon William Mazigo (Mtanzania) | Leseni ya *Condensate Dealership* |
| 75. | Edith Kibali Miaka Elfu Moja, S.L.P 92, Mtwara. | Eneo la Chikongola, Mtwara. | Amon Sengati (Mtwara) | Leseni ya Usambazaji wa Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 76. | Ahmad Ally Uheche T/A Uheche Filling Station, S.L.P 447, Masasi. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Mtapika, Masasi, Mtwara. | Ahmad Ally Uheche (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 77. | Sayona Fruits Limited, S.L.P 3030, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 1, Kitalu "A", Eneo la Mboga, Chalinze, Pwani. | Pawan Subhash Patel (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta kwa Matumizi Binafsi |
| 78. | Mwanza Huduma Company Limited, S.L.P 403, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 48, Eneo la Visiga, Kibaha, Pwani. | Zulfikar Esmail Nanji (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 79. | Camel Oil (T) Ltd - Misugusugu Petrol Station, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 5 & 6, Eneo la Misugusugu, Kibaha, Pwani. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 80. | Africa Energy Ltd, S.L.P 22786, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 477, Kitalu "E", Eneo la Ikwiriri, Rufiji, Pwani. | Edha Nahdi (Mtanzania) | Leseni ya kituo cha mafuta |
| 81. | Nyakyame Co. Limited - Kimanzichana, S.L.P 8326, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 27, Kitalu "B", Eneo la Kimanzichana, Mkuranga, Pwani. | Joseph Kyalo Mwita (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 82. | Gapco Tanzania Limited, S.L.P 9103, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 284011/93, Kitalu "61 & 62", Eneo la Makonde, Lindi. | Mamadou Ngo. (Raia wa Senegal) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 83. | Kassim Mohammed Abdallah T/A Najma Petrol Station S.L.P 33 Lindi | Kiwanja Na. 53-58, Kitalu "V", Eneo la Kenyatta Lindi. | Kassim Mohammed Abdallah (Mtanzania) | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

***Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.***

***Imetolewa na***
***Mkurugenzi Mkuu,***
***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji***





# Vibaka wawanyima usingizi wakazi Sirari

**Na Samson Chacha,** TARIME

WAKAZI wa Mji wa Sirari Mpakani, Tarafa ya Inchugu wilayani Tarime wameiomba serikali kupitia Jeshi la Polisi kushirikiana na wananchi kuwasaka waporaji ambao wamekuwa kero na kuongezeka kila siku.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti wakati wakizungumza na Nipashe, wakitaja uporaji huo kuhusisha mali za wananchi zikiwamo runinga, laptop, simu za mkononi pamoja na bidhaa za dukani ukomeshwe na kurejesha utulivu.

Mkazi wa Sirari, Mwita Sasi, alisema wakati wa maonesho ya kibiashara Afrika Mashariki zimeibiwa laptop saba zenye thamani ya Sh. milioni tatu katika banda la Rollen Kaloa pamoja na runinga.

Alisema pia waliiba Sh.500,000, huku vibanda vya maduka vikivujwa na mali za watu kuporwa bidhaa na mitaji yao.

"Tunaomba polisi kwa kushirikiana na viongozi wa vijiji, vitongoji na wananchi kufanya msako ili kuwabaini wahalifu hao ili wafikishwe kwenye vyombo vya sheria na kurejesha kwa wananchi," alisema Suzana Chacha ambaye ni mfanyabiashara.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kanisani, Nyamagige Gesamara, alikiri kuwapo kwa uporaji huo na kusema kuwa hapo awali doria za polisi kwa kushirikiana nasi na wananchi zilisaidia kuimarisha ulinzi na usalama kwa kuwabaini wahalifu na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mtendaji wa Kata wa Sirari, Wakuru Mrumbe, aliwataka viongozi kushirikiana na wananchi kulipatia Jeshi la Polisi ushirikiano katika kuwabaini wahalifu.



Mtia nia wa ubunge Jimbo la Kigoma Kusini kwa tiketi ya CHADEMA, Joseph Matata, akizungumza juzi, kabla ya kuendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa msikiti wa Taqwa ulioko Kata ya Nguruka, wilayani Uvinza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 400 Sekondari Maganzo wanakaa chini

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WALIMU na wanafunzi katika Shule ya Sekondari Maganzo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali pamoja na wadau wa elimu kuisaidia shule hiyo viti na meza ili kunusuru wanafunzi zaidi ya 400 wanaokaa chini.

Walibainisha hayo juzi wakati wa kupokea meza na viti 44 shuleni hapo, vilivyotolewa na Benki ya CRDB ili kupunguza adha hiyo inayotajwa kuwatatiza wanafunzi wakati wa masomo yao.

Makamu Mkuu wa Shule hiyo, Evalisti Luhende, alikiri kuwapo kwa uhaba wa samani hizo na kueleza kuwa shule hiyo ina jumla ya wanafunzi 1237, huku ikiwa na upungufu wa viti na meza 403.

Hivyo, alishukuru benki hiyo kwa msaada wa viti na meza na kusema utawasaidia kupunguza tatizo hilo na kurejesha utulivu wa wanafunzi wakati wa masomo yao na kuongeza ufaulu.

Mkuu wa kitengo cha malipo na udhibiti kutoka CRDB, Madaha Chabba, alisema wamekuwa na utaratibu wa kutenga asilimia moja ya faida ambayo wanaipata na kurudisha kwa jamii.

Alisema katika kurudisha faida kwa jamii wamekuwa wakitekeleza miradi mbalimbali, wakijikita zaidi katika sekta ya elimu ili kutatua matatizo mbalimbali yaliyoko ikiwamo upungufu wa vyumba vya madarasa.

Alisema katika shule hiyo wilayani Kishapu wameamua kukabidhi meza na viti 44 ili kupunguza upungufu mkubwa wa samani hizo uliopo kwa sasa.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Magharibi, Jumanne Wagana, alisema wamekuwa mstari wa mbele kusaidia jamii katika kutekeleza miradi mbalimbali inayolenga kuboresha elimu na kwamba Aprili, mwaka huu.

Pia walikabidhi vyumba viwili vya madarasa vikiwa na meza na viti katika Shule ya Msingi Kiloleli wilayani Kishapu.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kishapu, Fatma Mohamed, aliwataka wanafunzi kutumia vyema meza na viti hivyo kwa kusoma kwa bidii lengo ili kuongeza ufaulu shuleni hapo.

# TRA yataka mabadiliko ya kodi, sheria kuzingatiwa

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) mkoani Mara imewataka wafanyabiashara mkoani hapa kupitia na kuzingatia mabadiliko ya kodi pamoja na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2024, ili kusaidia kukuza pato la taifa.

Kauli hiyo imetolewa na Ofisa Mkuu wa Usimamizi wa Kodi, Elimu na Mawasiliano TRA, Geofrey Canova, wakati wa semina na wafanyabiashara iliyofanyika wilayani Tarime kuhusu mabadiliko hayo.

Alisema mabadiliko hayo yanalenga kuboresha ukuaji wa pato la Taifa, kudhibiti mfumuko wa bei, kuimarisha mapato ya ndani, na kuongeza akiba ya fedha za kigeni.

Aliyataja baadhi ya sheria zinazofanyiwa marekebisho kuwa ni pamoja na sheria za kodi ya mapato, ushuru wa bidhaa na usimamizi wa kodi.

Ofisa Kodi Mkoa wa Mara, Adolph Ntango, aliwakumbusha wafanyabiashara hao kuhakikisha wanashiriki kikamilifu siku ya elimu na utatuzi wa kero iliyotengwa Siku ya Alhamisi kwa ajili ya kuwasilisha malalamiko yao na kero.

Akieleza mabadiliko katika ada za usajili wa magari na tozo za marekebisho ya viwanda kwa bidhaa zinazoingizwa nchini, Ofisa Forodha Mwandamizi, Evodius Elias alisema jukumu la kukusanya mapato ya tozo za mizigo kwa Mamlaka ya Bandari.

Mmoja wa wafanyabiashara, Mordekai Moseti, alipendekeza kupunguzwa kwa ushuru wa bidhaa, hasa kwa baadhi ya vileo ili kupunguza mzigo wa kodi kwa wafanyabiashara.

## Wafanyabiashara waitwa kuwekeza mgodini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAFANYABIASHARA 150 wanaozunguka mgodi wa Barrick Bulyanhulu mkoani Shinyanga, wametakiwa kuchangamkia fursa za uwekezaji wa biashara, ili kunufaika na uwekezaji uliopo pamoja na kuinua uchumi wao.

Kaimu Meneja Mkuu wa mgodi wa huo, Victor Lule, alitoa wito huo juzi wakati wa utoaji wa mafunzo yaliyofanyika katika Kijiji cha Kakola Kata ya Bulyanhulu Msalala mkoani Shinyanga, kusema watayafikia makundi mengine ili yazidi kuchangamkia fursa zinazopatikana mgodini.

Wafanyabiashara hao walipewa elimu ya ujasiriamali itakayowawezesha kuchangamkia fursa za kibiashara na kunufaika na uwekezaji wa mgodi huo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Lule alisema wanaamini msingi wa maendeleo ndani ya jamii unatokana na watu na hatua stahiki kwenye fursa zinazopatikana.

Alisema ndiyo sababu ya kuwekeza katika programu hiyo ili kuwahamasisha wafanyabiashara kuzitambua fursa zinazopatikana ndani ya mgodi.

"Tangu programu hii tuianzishe tayari tumewafikia wafanyabiashara mbalimbali waliopo maeneo jirani na migodi ya Barrick North Mara na Bulyanhulu na yamewawezesha baadhi yao kuchangamkia fursa migodini na kupata mafanikio ya kibiashara, zinapotangazwa zabuni mgodini tunawapa kipaumbele kwanza waliopata mafunzo haya," alisema Lule.

Mmoja wa washiriki, Anastazia Ibrahim kutoka Halmashauri ya Nyang'hwale mkoani Geita, alisema matarajio yao siyo tu kuchangamkia fursa mgodini bali pia kupata ujuzi utakaowawezesha kuchangamkia fursa za kibiashara zinazojitokeza na kuendesha biashara zao kitaalamu na kufuata sheria za nchi katika kuuza nje.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita aliwataka wafanyabiashara kuchangamkia fursa ya mikopo ya asilimia 10 inayokwenda kutolewa hivi karibu.

Alisema mikopo hiyo itawasaidia kupata mitaji na kuendesha shughuli zao kupitia elimu watakayokuwa wameipata.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 3, 2024
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




## Ndivyo ukweli matumizi mkono wa kushoto unavyochanganya watafiti




Usitupe matunda wala makombo; ni fedha, protini ya kulisha mifugo




Ukimfuga sungura hakuna cha kutupa

ELIMU

NA DK. REUBENI LUMBAGALA, DODOMA

# Programu ya Tutunzane Mvomero darasa linalohitaji kusambaa kote

UKAME unaotokana na kukata miti ovyo kupata nishati, malisho na makazi yanayogeuza ardhi kuwa jangwa pamoja na athari za mabadiliko ya tabianchi yanawalazimisha wafugaji kuhama hama kusaka malisho huku wakisababisha migogoro kwa wakulima.

Ni jambo lililotesa wengi lakini sasa ni amani kufuatia ujio wa kampeni ya 'Tutunzane Mvomero-Mfugaji Mtunze Mkulima na Mkulima Mtunze Mfugaji ili Kulinda Mazingira Yetu."

Ni mradi unaoasisiwa na viongozi na kusimamiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mvomero, Judith Nguli, ukizinduliwa mwezi uliopita na Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Morogoro.

Kampeni hii ni darasa muhimu katika jitihada za kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji wilayani Mvomero kupitia kuwapa elimu makundi hayo mawili ili kuondoa uadui dhidi yao kwani kila mmoja anamtegemea mwenzie katika shughuli zao.

Mvomero ni sehemu ndogo ya Tanzania hii kubwa yapo maeneo mengi yenye migogoro ya ardhi huku yakichagizwa na ugomvi baina ya wakulima na wafugaji, elimu iliyo ndani ya kampeni hiyo ya tutunzane inapaswa kusambaa na kuvuka mipaka ikienea nchi nzima.

Kuwaelimisha na kuwahamasisha wakulima kutaihakikishia nchi amani na kumaliza ugomvi kati ya wakulima na wafugaji na kuchangia maendeleo kwani sekta



Rais Samia Suluhu Hassan akiwasalimia wakazi wa Kibaoni, Ifakara ikiwa sehemu ya ziara yake ya kikazi mkoani Morogoro. **PICHA: IKULU**

mbili hizo za kilimo na ufugaji ni muhimu katika maendeleo kwa vile ndiko kinapotoka chakula na malighafi viwandani.

Makundi haya mawili yanategemeana. Kwa mfano, anayefuga hawezi kuishi kwa kula nyama na maziwa pekee, vilevile mkulima hawezi kuishi kwa kutegemea mazao ya shambani kwake tu, kwani kuna wakati anahitaji nyama, maziwa na mifugo kutoka kwa wengine na huo ndiyo mlo kamili kama wanavyoshauri wataalamu wa lishe.

Lakini hata katika maisha ya kawaida, wakulima na wafugaji wanapaswa kuishi kwa amani kwa miaka mingi, makundi haya mawili wamekuwa ni ndugu wanaoishi pamoja na kufanya mambo mengi kwa ushirikiano wala hakuna aliye bora zaidi ya mwenzake kama kampeni inavyosema kutunzana kwa sababu wanahitajiana na wanategemeana pia.

Kutokana na ukweli kuwa, ardhi ni nyenzo muhimu ya kimaendeleo, ni lazima kuwe na matumizi endelevu ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara inayohatarisha amani na ustawi wa maendeleo kwa kuhakikisha wakulima wanakuwa na maeneo yao kwa ajili ya kilimo, hali kadhalika wafugaji nao ili kila kundi liepuke kuingia katika eneo la mwenzake.

Kampeni ya tutunzane imelenga kuhamasisha wakulima na wafugaji kurasimisha ardhi zao kwa gharama nafuu ili kupata hati miliki za mashamba yao, wapewe mbegu za malisho na mazao mengine ili kupanda.

Katika ardhi zao zilizopimwa, wafugaji watakuwa na uwezo wa kupanda malisho mazuri kwa ajili ya chakula cha mifugo yao na kuepukana na kadhia ya kwenda kulisha wanyama kwenye mashamba ya wakulima ambapo inaleta ugomvi, uhasama na kuwatia hasara wakulima kwa kupoteza mazao yao na hivyo kuendelea kuishi maisha duni.

Kampeni inasisitiza ufugaji wa kisasa, kuondokana na migogoro kati yao na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. "Kampeni hii ni muhimu kwa sababu inataleta amani, ongezeko la malisho, tija na wafugaji waweze kukopesheka," anasema Rais Samia katika uzinduzi.

Aidha, kampeni hii pia inachochea maendeleo kwa kuweka mkazo wa kuwa na eneo dogo lakini lenye uzalishaji mwingi unaotokana na teknolojia kwa kufuata mbinu za kisasa za kiuzalishaji kwani utaalamu unaonesha kuwa, ili kuwe na tija kwenye kilimo, hakuna haja ya kulima eneo kubwa au ili kuzalisha nyama na maziwa mengi si lazima kuwa na mamia ya mifugo.

Changamoto ya mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba dunia sasa hayana budi kukabiliwa kupitia mbinu za kisasa za kiuzalishaji:

"Lazima tuwe wabunifu wa kuja na mbinu zitakazofanya ardhi tuliyonayo izalishe zaidi. Kama ni mkulima avune kwa wingi kwa kipande cha ardhi alichonacho vivyo hivyo kwa mfugaji", anasema Rais Samia.

**R4 NDIYO TUTUNZANE**

Rais Samia anazungumzia falsafa yake ya R4 ya kwanza 'reconciliation' au maridhiano, 'resilience' au ustahimilivu, 'reform' ndiyo mabadiliko na 'rebuilding' au kujenga upya.

Kutokana na uwapo wa uhasama kati ya wakulima na wafugaji, kumekuwa na haja ya kuwa na maridhiano baina yao,

INAENDELEA UK. 13

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo ukweli matumizi mkono wa kushoto unavyochanganya watafiti

INAPOFIKA Agosti 13 ni maadhimisho ya siku ya kimataifa ya watu wanaotumia mkono wa kushoto.

Hata hivyo, haijafahamika ni kwa nini kuna uwezekano mdogo kwa baadhi ya binadamu wanaotumia mkono wa kushoto kutumia wa kulia.

Utafiti wa kisayansi wa matumizi ya mkono wa kushoto, unaonyesha taarifa nyingi zaidi kuhusu wanadamu, kuanzia jinsi unavyobadilisha namna ya kufikiria.

Aidha, kuna wale ambao wanaweza kutumia "upande wa kushoto," lakini mara hii kwa maana ya kusikia, na sio kwa mkono.

Yupo mtu anatumia mkono wa kushoto tangu utotoni, hasa wakati anapoanza kushikilia kitu na kushika kalamu kuandika kwenye karatasi.

**KUSHOTO NI BORA?**

Ni nini hufanya mkono mmoja kuutawala mwingine, na kwa nini watu wanaotumia mkono wa kushoto ni wachache?

Maelezo yanayohusiana na mada hii ni zaidi ya watu walivyofikiria. Kwa mfano, hatukutambua hapo awali kwamba utegemezi wa mtu kwa mkono mmoja zaidi kuliko mwingine ni jambo ambalo pia linaenea kwenye viungo vingine. Mfano macho.

Kila mmoja anaweza kutambua kama yeye ni mtumiaji wa mkono wa kushoto kupitia majaribio yafuatayo:

Kuna mfano wa kujaribu: Nyoosha mkono mmoja na ushikilie kidole gumba mbele yako. Kisha angalia kwa macho yote mawili na kisha kwa kila jicho wakati ukifunika jicho lingine.

Jicho lako lenye nguvu litakuwa lile linalokuruhusu kuona kidole karibu na muundo wake wa asili zaidi.

Unaweza pia kujaribu masikio yako ili kuona ni lipi unalotumia mara moja na kwa urahisi zaidi wakati wa kuongea na simu.

Ni jambo la kushangaza kuona haya yanatokea katika maisha halisi. Mara nyingi, wapo wanaoshikilia simu mkono wa kushoto na kuiweka kwa shida sikio la kulia, wakati unaandika haraka kwa na mkono wa kulia

Kwa ujumla, asilimia 40 ya binadamu husikia vizuri kwa sikio la kushoto, asilimia 30 wanaona vizuri kwa jicho la kushoto na asilimia 20 wana mguu wa kushoto wenye nguvu kuliko wa kulia.



Kuanzia mwaka 1976, kila Agosti 13, dunia inaadhimisha siku maalum ya watu wanaotumia mkono wa kushoto. Rais mstaafu wa Marekani, Barrack Obama ni baadhi ya watu mashuhuri wanaotumia mkono huo. **PICHA: MTANDAO**

Jambo la kushangaza ni kwamba asilimia ya chini sana linapokuja suala la wale ambao "wanatumia mkono wa kushoto", kwani asilimia yao haizidi 10 ya idadi ya watu.

KWA NINI?

Inasemekana hapo zamani waliokuwa wanatumia mkono huo walifokewa na kufukuzwa kwa sauti kubwa na kuonekana kuwa wanatia aibu.

Mfano wakiwa wanafunzi shuleni au kwenye shughuli za kijamii walichukuliwa kama watu walio kinyume na njia ya asili.

Hata leo hata hakuna maelezo mabaya yanayohusishwa na mkono wa kushoto ambayo bado yanaendelea katika lugha nyingine.

Neno la Kiingereza "kushoto" linatokana na lugha ya Waanglo-Saxon ambalo liliandikwa lyft na lilimaanisha "dhaifu."

Neno kinyume cha "kushoto" katika Kilatini ni 'dexter, maana yake "mkono wa kulia" na lilihusishwa na ustadi, uadilifu, ucha mungu, na haki.

Kwa hivyo ni nini kinachoamua kuwa mtu atakuwa anatumia zaidi mkono wa kushoto? Kwa mtazamo wa mabadiliko, ni rahisi zaidi kufahamu sababu za kutumia mkono mmoja kuliko mwingine.

Kwa upande wa nyani wana uwezo wa kugawa kazi fulani kwa mkono mmoja.

Sokwe huchagua "mkono" ambao anaona unafaa zaidi kati ya viungo vyake na kuuingiza kwenye shimo ambapo wadudu wanaishi, kwani hisia ya kugusa humpa habari nyingi juu ya kina na upana wa shimo na jinsi lilivyo na mchwa ambao wana ladha kwa aina hii ya tumbili.

Kisha sokwe huvuta "mkono" wake kwa urahisi, akifunua mawindo yake, ambapo hujaribu kulazimisha kuingiza taya shimoni.

Kwa kutumia mkono huo huo kufanya kazi hiyo, kila wakati hula mchwa wengi.

Lakini, utafiti uliofanywa na wanasayansi wa nyani na sokwe wa porini umeonyesha kuwa matumizi yao ya viungo ni tofauti na binadamu.

Katika kila kazi ambayo watafiti waliifanya kuwahusu sokwe, ilionyesha kuwa nusu ya sokwe walitumia "mkono wa kulia" kuifanya, wakati nusu nyingine walitumia wa kushoto, yaani, uwiano wa asilimia 50 kwa 50, ambayo inaleta swali.

Katika hatua gani kwenye mageuzi yetu wale wanaotumia mkono wa kulia kimsingi walionekana kuwa wengi zaidi kuliko wenzao wa mkono wa kushoto? Mtu mmoja kati ya 10 anatumia mkono wa kushoto?

Meno ya binadamu wa kale 'Neanderthals' ni kiashiria muhimu katika suala hili. Inaonekana kuwa mtu huyu alikuwa na akili na mwenye busara kwa wakati mmoja.

Mababu hao walitumia meno yao kushikilia vipande vya nyama ili kuzikata kwa kisu kilichoshikiliwa mkono wa kulia.

Alama hii ya kushoto kwenye meno ya mbele na kwa kuchunguza alama hizi, wanasayansi waliamua ni mkono gani ulioshikilia kisu na ambao ulishikilia nyama.

La kushangaza, uchunguzi huo ulifunua kuwa uwiano wa mkono wa kushoto na wa kulia kati ya wanadamu hawa wa zamani ulikuwa sawa na uwiano kati yao leo, mmoja hadi 10.

Hata hivyo, inajulikana kwamba kuna msingi wa maumbile. Hata hivyo, wanasayansi katika uwanja huu bado wanajaribu kutambua sehemu maalum za nasaba (DNA) zinazohusika na hili, na idadi ya jeni zinazoaminika kuwa na jukumu katika suala hili kufikia jeni 40 tofauti.

Kwa kuzingatia data ya sasa, hatuwezi kujua sababu maalum kwa nini watu wengine wanatumia mkono mmoja zaidi kuliko mwingine, wala hatuna maelezo ya ni kwa nini "watu wa wanaotumia mkono wa kushoto" ni wachache. Kwa hivyo, jibu la swali lolote katika suala hili linabaki kuwa "halijapatikana."

Lakini je, kutumia mkono wa kushoto kuna athari yoyote kwa maisha ya mtu, isipokuwa ugumu? Sivyo, katika kushika mkasi ambao umeundwa kwa matumizi na mkono wa kushoto au zipu ambayo mtu hawezi kuifunga, au kalamu ambayo inashikika vizuri kwa mkono wa kulia? Hakuna jibu.

SAYANSI

**NA SABATO KASIKA**

# Usitupe matunda wala makombo; ni fedha, protini ya kulisha mifugo

MATUMIZI ya protini kama dagaa na soya kulisha wanyama yanaongezeka. Hata hivyo, vyakula hivyo pia hutumiwa na binadamu, jambo linaloongeza ushindani, mahitaji na gharama sokoni.

Ubunifu ni njia mojawapo inayoweza kutumiwa kupata bidhaa hizo kama jamii itafundishwa jinsi ya kutumia malighafi zilizopo ili kupata protini na vyakula vingine vya kulisha wanyama.

Ubunifu upo wa aina nyingi, lakini kwenye eneo la protini za mifugo Juma Masanja, anaeleza namna ya kuzalisha protini kwa kutumia maganda ya matunda na mabaki ya vyakula kwa ajili ya wanyama na kuku ili kuboresha afya zao.

Anasema chakula hicho huzalishwa kwa kutumia maganda ya matunda na vyakula vinavyobaki au makombo kuanzia ugali, maharage, wali na mboga ambavyo baada ya kukusanywa na kuwekwa mahali kwa muda mfugaji anapata funza wa kulisha wanyama.

Anasema miongoni mwa matunda ni matikiti maji, mafenesi, maembe, ndizi, maparachichi, lakini pia maganda ya viazi, mabaki ya mboga za majani na makombo.

Mtaalamu huyo wa kuzalisha funza hao Masanja kutoka Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni jijini Dar es Salaam, anazungumza na Nipashe hivi karibuni akitaja mbinu anazotumia kufikia lengo hilo.

Ni katika mafunzo ya jinsi ya kutumia taka hizo kwa tija yanayotolewa na kituo hicho kwa vikundi vya uzalishaji mali vya kata za Majohe na Kivule ili kuondoa umaskini na kuboresha maisha.

Masanja anasema, ili kupata wadudu hao, malighafi hizo zinakusanywa, kujazwa katika ndoo ya lita 20 na kuachwa kwa wiki tatu ili wadudu hao wapatikane.

"Baada ya siku 21, wadudu waitwao 'black soldiers' wamezalishwa na wako tayari kuvunwa kwa ajili ya kulisha ng'ombe, nguruwe au kuku. Wanaprotini nyingi zinazowafanya wanyama kunenepa," anasema Masanja.



Wajasiriamali Kipunguni wakiandaa matunda na makombo ili kuzalisha wadudu au protini ya kulisha mifugo.



Wadudu (black soldiers), walio tayari kulishwa na kuku, bata na nguruwe. **PICHA ZOTE: SABATO KASIKA**

Mtaalamu huyo anafafanua kuwa, kilo 100 za taka hizo, zinaweza kutoa kilo moja ya wadudu hao, na kwamba ndoo moja ya taka inavunwa mara tatu kila baada ya siku 21.

Anaeleza kuwa, wanaweza kukaushwa au kulishwa mifugo wakiwa wabichi.

Masanja anasema, kilo moja ya wadudu hao inachanganywa katika kilo 20 za pumba wakiwa wabichi au wakawa wamekaushwa na kuwalisha ng'ombe, nguruwe au kuku.

Wadudu hawa wanavunwa mara tatu kila baada ya siku 21, kabla ya kubadilisha taka. Vilevile, taka zikishamaliza muda wake wa kuzalisha wadudu, zinatumika ni mbolea," anasema.

Anaeleza kuwa, kwa kutumia ubunifu huo, kituo kinapunguza uchafuzi wa mazingira kwenye jamii, hasa kupitia taka ambazo wanazizalisha wadudu hao, kwa ajili ya lishe ya mifugo.

Katika maelezo yake zaidi, anasema wameamua kuingiza taka kwenye mnyororo wa thamani, kwa kuzitumia kuandaa chakula ambacho kinajenga afya ya mifugo, lakini pia kutumika kama mbolea kwenye bustani, badala ya kuzitupa.

"Wakati tunaanza kuzalisha wadudu hawa, tulikuwa tunauza kilo moja kwa shilingi 10,000, lakini kwa sasa tunauza kilo moja kwa shilingi 5,000 ili kuvutia wateja wengi zaidi," anasema.

Aidha, Masanja anasema; "Nilipata elimu kutoka Taasisi ya Utafiti na Matibabu Afrika (AMREF) ya jinsi ya kuutumia taka kuzalisha funza wenye virutubisho, kwa ajili ya ya lishe kwa mifugo. Nimeileta kuingiza taka katika mnyororo wa thamani kwa kuzitumia kupata chakula cha wanyama," anasema.

Beatrice Oswald kutoka Kivule anazungumzia mafunzo hayo, akisema yana manufaa mengi ikiwamo kupunguza uchafuzi wa mazingira, iwapo utazingatiwa na kila mdau.

"Kwanza unasaidia usafi wa mazingira, kwani mara nyingi taka za majumbani mwetu zinatokana matunda na hata mabaki ya chakula," anasema Beatrice.

Anasema badala ya kutupa taka hizo, sasa atazitumia kuzalisha wadudu hao na pia kwa ajili ya mbolea ambayo ataitumia katika bustani yake ya mboga, kwa kuwa haina gharama.

"Unaweza kwenda kwa mtu kuhitaji mbolea ya samadi ukauziwa, lakini hii ya maganda ya matunda hawezi kuuziwa, kwani hizo ni taka. Hivyo, ninakwenda kutumia kwa mambo mawili, kuzalisha wadudu na pia kupata mbolea," anasema.

Beatrice anasema, elimu aliopata haitaishia kwake, bali taipeleka kwa wenzake ili nao waone umuhimu wa kuzalisha wadudu, kwa ajili ya kuboresha afya ya mifugo yao.

Anafafanua kuwa, wamefundishwa kwamba kilo moja ya wadudu hao inauzwa Sh. 5,000, na kwamba mtu anaweza kufanya biashara ya kuwavuna na kuuzia wafugaji au kuwalisha mifugo wake na kutumia kama mbolea.

Amina Omary kutoka Majohe anasema, licha ya kuhisi kinyaa baada ya kuona wadudu hao, itabidi abadilishe mtazamo ili aende kulingana na fursa za kiuchumi zilizoko.

Anasema, ataendana na mazingira, asipitwe na wakati, kwa kuwa maisha yanakwenda mbio na ubunifu katika vitu mbalimbali unazidi kuongezeka kila kukicha.

Mjasiriamali huyo anasema, kwa kutumia malighafi hizo ambazo ni nyingi na rahisi kupatikana sokoni na hata nyumbani, usafi wa mazingira utaimarika.

***Usikose simulizi zaidi Alhamisi***

## PROGRAMU YA TUTUNZANE MVOMERO DARASA LINALOHITAJI KUSAMBAA KOTE

**INATOKA UK.11**

kwa kuweka mikakati madhubuti ikiwamo kampeni na elimu ya tutunzane ili kuleta amani.

Kampeni inasisitiza umuhimu wa kuleta mabadiliko kwa kulima na kufuga kisasa ili kuondoa migogoro na kuchochea maendeleo.

Vilevile, kampeni hiyo inalenga kujenga upya mahusiano mazuri baina ya wakulima na wafugaji kwani makundi haya yanahitajiana katika maisha ya kila siku.

Kwenye uzinduzi wa kampeni hiyo, Rais Samia anawaita mbele wawakilishi wa wakulima na wafugaji akawapatanisha kwa kuwaambia washikane mikono kama ishara ya kumaliza tofauti zao na kuanza ukurasa mpya.

"Mlime, wanaolima na mfuge wanaofuga, na kwamba tunategemeana wote. Ninyi ndiyo mnaotupa sisi uhai, mnatupa vitowe, chakula, hakuna haja ya kugombana, kuuana, wote ninyi ni wanadamu" anasisitiza Rais Samia.

Hili ni darasa la kujifunza kuwa na amani na maelewano lisambae wilaya nyingine ili kujifunza kutoka Mvomero waasisi wa kampeni ya tutunzane, ili kupunguza wingi wa kampeni tutunzane iwe ya kitaifa kwani ina manufaa mengi na imegusa maeneo mengi ya kimaendeleo. Sekta za kilimo na ufugaji zinategemewa katika ukuzaji uchumi na kutoa ajira nyingi kwa wananchi, hivyo zisikie anachosema Rais zifanye kazi bila migogoro na zione matunda.

***Mwandishi ni mwalimu wa Sekondari ya Mlali ya mkoani Dodoma. Maoni: 0620 800 462.***

ELIMU

NA PILLY KIGOME

# Ukimfuga sungura hakuna cha kutupa

## • Kuanzia samadi, mkojo hadi manyoya ni pesa



Sungura wakiwa bandani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

SUNGURA ni miongoni mwa wanyama wenye nyama iliyo na protini nyingi, isiyo na mafuta tofauti na kitoweo kingine kama cha ng'ombe na mbuzi.

Habari njema zaidi ni kwamba huchukua muda mfupi kukomaa, takribani miezi minne hadi sita, hivyo anayefuga kwa biashara anaanza kunufaika.

Nipashe, inapotembelea kampuni ya Saore iliyofanya shughuli zake Dar es Salaam, Arusha na Dodoma, inapata mengi ya kujifunza kutoka kwa mfuga sungura Juma Hassan, aliyefanya kazi hiyo kwa zaidi ya miaka 10.

Anasema teknolojia imerahisisha kila kitu kama kupatikana maarifa na taarifa, elimu na mbinu mbalimbali za kibunifu na kutunza mifugo ya kila aina.

Mfugaji huyo anasema sungura ana sifa nyingi na kwamba kila kitu katika mwili wake ni faida kwa binadamu, akieleza kuwa ana uwezo wa kuzaa watoto sita hadi 16 kwa mkupuo, akibeba mimba ni siku 28.

Hassan anafafanua kuwa, anaweza kuzaa kila mwezi asipopangiliwa uzazi hivyo ni mnyama ambaye kwa mwaka anaweza kuwa na watoto zaidi ya 100 ikilinganishwa na wanyama wengine wa nchi kavu duniani.

Mtaalamu huyu ambaye ni Meneja wa Kampuni ya Saore inayofuga sungura, anasema lengo lake ni kufuga kisasa na pia kuwasaidia maarifa na ujuzi watu wanaotaka kufuga wanyama hao.

FAIDA

Hassan anasema mnyama huyo kila kilichopo mwilini mwake kuanzia mkojo, ngozi ni dhahabu kama si utajiri.

Anasema mkojo wa mnyama unatengeneza mbolea za kustawisha mboga na mimea inayovunwa kwa muda mfupi kama mahindi, ni kiuatilifu kikichanganywa na vitu fulani huua visumbufu kadhalika ni 'buster' ikiwekwa kwenye majani mmea unakua kwa kasi.

" Ni habari njema kwa kuwa samadi ya mnyama huyu inatumika kutengenezea chakula cha samaki ambapo chakula hicho kinamfanya samaki kustawi na kumjenga awe mwenye afya bora," anasema na kuongeza kuwa chakula hicho kinachanganywa na viambato vingine.

Hassan anasema manyoya na ngozi ya mnyama huyu pia ni faida kubwa kwa binadamu katika kuukuza uchumi wake kwa kuwa ngozi hiyo ni malighafi hasa katika viwanda na mtu mmoja mmoja.

Manyoya hutumika kwa mapambo na ngozi nayo hutumiwa kutengeneza viatu,



pochi na mikanda, anaeleza mfugaji huyo.

Akizungumzia nyama ya sungura anasema ina faida ni nyama nyeupe ambayo haina athari, ikilinganishwa na nyama nyekundu hasa ya ng'ombe na mbuzi.

Inawafaa watoto, watu wenye mzio na pia inashauriwa kutumiwa na wenye kisukari na haina tindikali ya 'yuriki' (uric acid) inayosababisha magonjwa ya mifupa ya misuli ya 'gauti'.

"Nyama ya sungura ni ghali na soko lake kubwa ni China, Uswizi, Japan na Austaralia," anasema Hassan.

Akizungungumzia kuhusu ufugaji anasema wako wachache na idadi kubwa haivutiwi au kuogopa kufuga sungura na kukimbilia kuku, mbuzi, ng'ombe na nguruwe, wakiamini kuwa hawatapata matokeo bora kifedha, wakati si hivyo.

Anabainisha kuwa kampuni ya Saore inawasaidia wanaotaka kuwafuga kwa kuwapa elimu ya ufugaji na kuwasaidia mbinu na njia za kumtunza mnyama huyo.

Saore, anasema inawapatia wafugaji mbegu kwa unafuu lakini pia ni wanunuzi wa nyama ya sungura hivyo wakitoa mbegu wananunua pia tena kwa wakulima hao.

"Mfugaji anaponunua mbegu kwenye kampuni yetu atafahamu soko la sungura anaozalisha kwani tunampatia mwongozo wa masoko na biashara." Anasema Hassan.

Kwa kuona umuhimu wa wanyama hao, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, mwaka 2020 iliandaa Mwongozo wa Ufugaji Bora wa Sungura Tanzania.

Kwa mujibu wa mwongozo huo sungura ni mnyama mwenye asilimia 21 ya protoni ikilinganishwa na kuku mwenye asilimia 18.

Aidha, unawahamasisha wakulima na wafugaji ukiwaeleza kuwa unahitaji eneo dogo kwa ajili ya ufugaji na siyo mifugo inayotumia gharama kubwa kutunza.

"Sungura ana nyama nyeupe isiyo na mafuta wala lehemu, hivyo watalaamu wa afya huiita nyama tiba," unasema mwongozo huo na kuongeza kuwa bei ya mnyama huyo ni kuanzia shilingi 5,000 hadi 50,000 kutegemea soko.

Mtandao wa Access Agriculture, unazungumzia sungura ukisema, ni rahisi kufuga na huhitaji nafasi ndogo lakini unaweza kuwa na changamoto ya kupata masoko.

"Ingawa sungura wanazaana kwa haraka, wakulima wanaweza kupata ugumu kuwauza pamoja na nyama yao, lakini kwa kutumia ubunifu wanaweza kuandaa soseji ya sungura na kuongeza mapato," unaeleza mtandao huo.



# Waziri acharuka uzembe ajali barabarani, atoa agizo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani limetakiwa kuongeza udhibiti kwa madereva wazembe ambao wamekuwa chanzo cha ajali zinazotokana na kuendesha bila kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile, alitoa maagizo hayo juzi jijini hapa wakati akifunga kilele cha Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani na Maadhimisho ya miaka 50 ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani.

Alisema Kikosi cha Usalama Barabarani kinatakiwa kuongeza udhibiti kwa madereva wazembe kwa kuchukua hatua kali za kisheria kwa watakaobainika kusababisha ajali kwa uzembe.

Aidha, alikitaka Kikosi cha Usalama Barabarani kuongeza nguvu kwenye ukaguzi wa magari yote mara kwa mara badala ya kusubiri wakati wa matukio kama hayo.

Alisema malengo makuu ya maadhimisho hayo ni kuwakumbusha wananchi na umma kwa ujumla kuhusu matumizi sahihi ya barabara ili kupunguza ajali.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani ambaye ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Nchini, Ramadhani Ngázi, alisema kuwa katika maadhimisho hayo elimu ilitolewa kwenye shule za msingi na sekondari na vituo vya waendesha bodaboda.

Alisema mikakati ni kufikia kundi la waendesha bodaboda ambao ni usafiri unatumiwa na wananchi walio wengi.

Mjumbe wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, Naibu Kamishna wa Jeshi la Polisi Mstaafu, Mohamed Mpinga alisema katika maadhimisho hayo mpango mkakati wa miaka mitatu wa kudhibiti ajali nchini ulizinduliwa.

Alisema lengo la mkakati huo ni kupunguza ajali kwa asilimia 50 kutoka ajali 1,643 hadi 822, pia kupunguza majeruhi kutoka 2,689 hadi 1,344 ifikapo mwaka 2030.

Alisema wakati wa maadhimisho hayo walitembelea shule sita za msingi ikiwamo Uhuru, Makole, Mlimwa, Kizota, Kisasa na Chaduru kwa ajili ya kutoa elimu.

Mhandisi kutoka Wizara ya Ujenzi, Omar Kinyera, alisema wako katika hatua ya kufanya mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani ili kubadili baadhi ya mambo yamebadilika ili ifikapo mwaka 2030 vifo viwe vimepungua kwa asilimia 50.

## Madereva bodaboda 200 wapewa elimu ya usalama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na ongezeko la ajali nchini zitokanazo na pikipiki, Chuo cha Udereva cha Wide Institute of Driving cha jijini Dodoma kimetoa mafunzo ya usalama barabarani kwa madereva bodaboda 200.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa chuo hicho, Faustine Matina alisema lengo ni kusaidia kupunguza ajali.

Alisema chuo hicho katika kipindi cha wiki ya nenda kwa usalama barabarani kimeandaa mafunzo hayo kwa madereva bodaboda 200, ambao wamejengewa uwezo kuhusu Sheria ya Usalama Barabarani ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikisababisha vifo na ulemavu wa kudumu.

Aidha, aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama za leseni kwa waendesha pikipiki ili kuwasaidia wengi kuwanazo ili kukomesha tabia ya baadhi ya watu kuendesha vyombo vya moto bila kuwa na leseni.

"Tunaomba serikali iangalie gharama za leseni kwa ajili ya bodaboda zipunguzwe haiwezekani leo mtu anayeendesha basi la watu 70 gharama ziwe sawa na mtu wa bodaboda, lakini sisi baaada ya mafunzo haya wote ambao hawana leseni tunaandaa utaratibu wa kukopesha leseni ambazo watakuwa walipa kidogokidogo," alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Elimu ya Usalama Barabarani nchini ACP, Michael Deleli, alikipongeza chuo hicho kwa kutoa mafunzo hayo, huku akiwataka madereva pikipiki kuzingatia sheria za usalama barabarani wakati wote.

Kadhalika, alikemea vitendo vya madereva hao kuendesha pikipiki ambazo zimeondolewa vioo vya pembeni ama kufungwa honi za malori ambazo zinakuwa kero kwa watumiaji wengine wa barabara.

**Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mkurugenzi wa chuo hicho, Faustine Matina alisema lengo ni kusaidia kupunguza ajali.**



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Manyoni, Jumanne Makhanda, akitoa maelekezo juzi kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Handu, Halmashauri ya Itigi, Yusuph Bakari, baada ya kukagua ujenzi wa darasa moja katika shule hiyo. Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Manyoni inafanya ziara katika kata zote kukagua miradi ili kuangalia utekelezaji wa ilani ya CCM. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kufilisika chanzo wanaume kupigwa na wake zao Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANAUME kuyumba kiuchumi na kushindwa kuwajibika katika malezi ya familia kunasababisha kupigwa na wake zao katika Tarafa ya Ilongero Halmashauri ya Wilaya ya Singida mkoani hapa.

Hayo yamebainishwa na shirika lisilo la kiserikali la WELAO ambalo linajishughulisha na uwezeshaji wanawake elimu ya kisheria na msaada wa kisheria ambalo linafanya kazi katika mikoa ya Tanzania Bara.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Innocencia Mkenga, akizungumza jana katika mahojiano na Nipashe alisema matukio ya wanaume kupigwa na wake zao yanaripotiwa zaidi katika Tarafa ya Ilongero na Mtinko mkoani Singida.

Mkenga alisema shirika hilo limebaini sababu za wanaume kupigwa mara nyingi inatokea mwanamke akiwa na hela kumzidi mwanaume, wivu wa mapenzi, matunzo kwa familia na baadhi ya wanawake kuwa na sauti kuliko mwanaume.

Alisema hadi kufikia Julai mwaka huu shirika hilo limeweza kuhudumia wateja 450 wakiwamo wanawake 255 na wanaume 195 ambao wanahitaji msaada wa kisheria.

Aliongeza kuwa katika matukio ya wanaume kupigwa zipo kesi tatu ambazo zimemalizika hivi karibuni mahakamani na za wanawake kupigwa zipo mbili na hivyo kufanya jumla ya kesi zilizopo mahakamani kuwa ni 505.

Mkenga aliwataka wanaume wanaponyanyaswa na wake zao wasisite kwenda kutoa taarifa ili waweze kusaidiwa kisheria badala ya kunyamaza kimya.

Alisema shirika hilo pia linajishughulisha na kupambana na mabadiliko ya tabia ya nchi, HIV na kifua kikuu ambapo kwa mwezi wagonjwa wapya wa VVU wamekuwa wakiibuliwa kwa mwezi.

## Wanafunzi sekondari wapewa elimu matumizi ya fedha

**Na Gwamaka Alipipi**

KATIKA kudhibiti matukio ya wananchi kujiingiza katika mikopo umiza, Wizara ya Fedha kupitia Hazina Sacoss wametoa elimu ya akiba, mikopo na fedha kwa wanafunzi zaidi ya 1,000 wa shule za msingi jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Hazina Saccos, Festo Mwaipaja, alisema hivi sasa wananchi wengi wamejiingiza katika mikopo yenye riba kubwa kutokana na kutokuwa na elimu ya fedha.

Alisema kutokana na hali hiyo wamelazimika kuanza kutoa elimu kwa wanafunzi wa sekondari ili jamii ielewe namna ya kuepuka na janga hilo.

"Tumeamua kuwajengea uwezo wa elimu ya fedha watoto wa shule za sekondari ili wakienda chuo kikuu wawe na uwelewa hata wakipewa mikopo. Sasa hivi malalamiko ni mengi kwa wananchi kuhusu mikopo umiza," alisema.

Alisema wanafanya hivyo ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan katika kupambana na ujinga na umaskini, kwamba elimu hiyo wataipeleka mikoani.

Naye Katibu Mkuu wa Hazina Saccos, Daniel Mwakyambiki alisema wametoa elimu ya fedha na mikopo katika shule mbalimbali kwa kuanzisha klabu.

Alizitaja shule hizo ni Tambaza, Kisutu, Minazi Mirefu, Kinyerezi, Migombani, Kigogo, Mzimuni, Turiani, Kambangwa na Makumbusho.



# NFRA yapewa siku saba kuondoa mahindi

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dk. Hussein Omar, amewataka Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Makambako kuhakikisha ndani ya wiki moja mahindi yaliyonunuliwa na Shirika la Kimataifa la Miradi ya Chakula (WFP) yanaondolewa, ili kupata nafasi ya kuhifadhi mahindi yanayonunuliwa kutoka kwa wakulima.

Alitoa agizo hilo juzi katika Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani Njombe alipokuwa katika ziara ya ukaguzi wa ununuzi wa mahindi ya wakulima sambamba na kusikiliza kero na kuzitatua.

"Hapa nimekuta changamoto ya kuchukuwa muda mrefu kumwaga mahindi, kwa hiyo maelekezo yangu kwa NFRA kwanza kuna mzigo wa WFP kwa hiyo ni kuangalia mkataba ili wachukue mahindi yao, kuweza kupatikana nafasi ya kuongeza mzigo mwingine na utaratibu wa kumwaga mahindi liende kwa haraka," aliagiza Dk. Omar.

Alisema mavuno ya mwaka 2024 yameongezeka ukilinganisha na miaka mingine, kutokana na wakulima kutumia mbolea za ruzuku.

"Ruzuku hii ambayo tumeweza kuitoa miaka miwili mfululizo na mwaka huu unaenda kuwa mwaka wa tatu wanasema imejibu kwa maana uzalishaji umeongezeka, tulikuwa tunazalisha tani 1.7 kwa hekta moja," alisema.

Alifafanua kuwa: "Lakini sasa hivi wakulima wanazalisha tani mbili kwa hekta moja kwa hiyo wakulima wana mahindi mengi sana hiyo ilikuwa ni lazima tuwahakikishie soko".

Naye Meneja wa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Makambako, Revocatus Bisama alisema kuanzia Julai mwaka huu hadi hivi sasa wamefanikiwa kununua tani 18,000 za mahindi, huku wakiwa na lengo la kununua tani 66,000.

Alisema: "Tani 66,000 tulizowekewa kama malengo tutazifikia lakini mimi malengo yangu ni kufikisha tani 100,000 na nina uhakika mahindi ni mazuri, wakulima wanazidi kuleta mahindi na tutayanunua ili kufikia lengo hili".

Awali baaadhi ya wakulima akiwamo, Yusto Kiyeyeu aliiomba kuongezwa nafasi ili mchakato wa uuzaji wa mahindi ufanyike kwa wepesi na haraka.

Mkulima mwingine, Fedrick Mkinga, alisema ili waweze kuzalisha mahindi yenye ubora ni vema serikali ikajipanga, ikaja na mkakati wa kutoa elimu kwa wakulima hasa maeneo ya vijijini, ili wasikutane na shida kama fangasi wanapokwenda kwenye masoko.



Baadhi ya mama na babalishe wa Jiji la Mbeya walioshiriki Tamasha la Mapishi la Tulia Cooking Festival, wakichukua bidhaa kwenye soko la mfano lililokuwa limeandaliwa na Taasisi ya Tulia Trust juzi, wakati wa fainali ya tamasha hilo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## RC akoshwa ushiriki wa NGOs katika maendeleo

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MKUU wa Wilaya ya Songea, Kapenjama Ndile , amesema mashirika yasiyo ya serikali mkoani Ruvuma yanamchango mkubwa wa maendeleo katika sekta mbalimbali.

Alisema hayo juzi katika jukwaa la mwaka la mashirika yasiyo ya kiserikali lililofanyika katika ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Songea, akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Ndile aliyataja mashirika hayo kuwa ni muhimu katika sekta ya maendeleo, kwamba aliyataka kufanya kazi kwa kufuata kanuni, taratibu na miongozo ya serikali ili kufanya kazi bila ya kuvunja sheria.

"Mnapotekeleza majukumu yenu zingatieni uwazi, uwajibikaji, kuripoti kwa wasajili wasaidizi ngazi ya mkoa na halmashauri, na kupeleka taarifa ya mpango wa bajeti ya shirika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa," alisisitiza Ndile.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Mary Makondo, aliyaomba mashirika yote yasiyo ya kiserikali kuhakikisha yanatambulika na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ili kuhakikisha ustawi na usalama wa jamii na Watanzania kwa ujumla.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa mashirika yasiyo ya kiserikali Mkoa wa Ruvuma, Aidan Mbilinyi, alisema wamejipanga kuhakikisha mashirika hayo yanafuata matakwa ya serikali, ili kuweza kuratibu kazi zao kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa.

Mkoa wa Ruvuma una mashirika yasiyo ya kiserikali 182 ambayo yamesajiliwa kisheria na mashirika saba ya nje yanayofanya kazi katika Wilaya na Halmashauri ya Mkoa wa Ruvuma yakijishughulisha na shughuli mbalimbali kama afya, elimu na kilimo.

# Watoto yatima 100 Njombe wakatiwa bima ya afya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATOTO yatima 100 kutoka vituo vinne vya Halmashauri ya Mkoa wa Njombe wamepatiwa kadi za bima ya afya zitakazowasaidia kupata huduma za afya za uhakika.

Msaada huo umetolewa na Kwaya ya Mtakatifu Mbaga Tuzinde na ulilenga kusaidia watoto yatima katika vituo hivyo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi kadi hizo juzi kwa viongozi wa vituo hivyo, mlezi wa kwaya hiyo, Deogratius Mtewele, alisema katika tamasha la mwaka 2023 waliomba michango kwa ajili ya kukata bima za afya kwa ajili ya watoto yatima 100 waliopo kwenye vituo.

"Tunashukuru kwa michango yenu kwa sababu inakwenda kusaidia huduma muhimu kwa watoto wetu hawa ambao hatima ya maisha yao inatutegemea sisi," alisema Mtewele.

Hata hivyo, Mtewele alivitaja vituo hivyo kuwa ni, Compassion Foundation watoto 40, Imiliwaha watoto 17, Ikonda Udiakonia watoto 17 na Kipengele watoto 26.

Mwenyekiti wa kwaya hiyo, Tarcisius Mdendemi alisema hivi karibuni walifanya ziara ya kutembelea vituo vya watoto yatima na wakabaini kwamba jamii inapeleka mahitaji mbalimbali ikiwamo chakula lakini siyo suala la kiafya.

"Mmoja wa wahudumu katika moja ya kituo tulichotembelea alisema kuna kipindi walilazwa zaidi ya watoto 20 ambapo ilihitajika gharama kubwa ya fedha ya kuwalipia hospitali, lile jambo lilitugusa sana ndipo tulipokuja na hili suala la kuwakatia bima za afya," alisema Mdendemi.

Baadhi ya watoto yatima akiwamo Pascal Mwinuka na Sarah Mlowe walishukuru kwa kupatiwa msaada wa bima za afya na kueleza kuwa zitawasaidia kupata matibabu ya uhakika.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kituo cha Compassion Foundation, Sister Lucia Mlowe aliwashukuru kwaya ya Mt. Mbaga Tuzinde kwa kuwahamasisha waumini na watu wenye mapenzi mema kuweza kuchangia fedha ambazo zimeweza kukata bima za afya.

Alisema: "Bima hizi zitatusaidia sana katika kuwatibu watoto hawa, kwa sababu kwenye vituo pekee kuwatibu watoto hawa kwa fedha kutoka mifukoni siyo kazi rahisi lakini kupitia bima hizi imetupunguzia mzigo mzito kwetu sisi na walau zile fedha tutazielekeza kwenye matumizi mengine".

Paroko wa Parokia ya Njombe Mjini, Padri Fransis Chengula aliitaka kwaya hiyo kuendelea kufanya matendo mema kwa sababu inaamsha jamii ya Watanzania kuwa na jicho la huruma kwa wahitaji.

## Mambo manne yatawala wagombea ubunge EALA

■Gladness Salame aibuka mshindi

**Na Grace Mwakalinga**

MASUALA ya kilimo, ajira, umaskini, mabadiliko ya tabianchi yamepewa kipaumbele kwa wagombea wanaowania nafasi ya ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), wakati wakinadi sera zao na kuomba kura kwa wajumbe wa Chama Cha Mapinduzi CCM, mjini Dodoma.

Kikao cha kupiga kura na kumchagua mgombea wa Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki kiliongozwa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi CCM, Kassim Majaliwa, ambaye ni Waziri Mkuu.

Katika kunadi sera zao wagombea hao walisema wakitapata nafasi watahakikisha wanaboresha sekta ya kilimo kwa kuhamasisha uzalishaji wenye tija ili wakulima wanufaike.

Mgombea Gladness Salame, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, aliwaomba wajumbe kumchagua kwa sababu ameshiriki katika kuandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2050 ambayo imesheheni masuala mbalimbali ikiwamo suala la kilimo, aliahidi kusaidia taifa kupatikana kwa masoko ya uhakika kulingana na mazao wanayozalisha.

Aidha, aliahidi kushughulikia suala la ajira kupitia fursa mbalimbali za kibiashara, kilimo na uwekezaji unaopatikana nchini, alisema endapo atachaguliwa atahakikisha anafungua fursa kupitia sekta mbalimbali ili kuzalisha ajira.

Aliyewahi kuwa Miss Tanzania, Queen Elizabeth Makune, aliahidi endapo atachaguliwa atafungua fursa za ajira kwa vijana kupitia sekta mbalimbali zinazopatikana ukanda wa Afrika Mashariki ikiwamo utalii.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Moshi, Prof. Neema Pumbulu, alisema akichaguliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki atasaidia kutengeneza sera na sheria kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi, atakuwa kiunganishi katika ya nchi za Afrika Mashariki na atahamasisha uhifadhi mazingira.

Mgombea Fatma Kange, aliahidi kushughulikia sekta ya kilimo kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika kuongeza thamani ya mazao ambayo alisema yatauzwa kwenye nchi mbalimbali za ukanda wa Afrika Mashariki.

Mgombea Dk. Hawa Mkwela- Mhadhiri wa Chuo cha Dodoma, aliahidi kutunza falsafa za Rais Samia Suluhu Hassan ya 4R, katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye Bunge la Afrika Mashariki.

Mgombea Fatma Msofe, aliahidi kuhakikisha masuala ya usawa wa kijinsia yanapewa kipaumbele na kufungua fursa za uwekezaji, kibiashara kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Theresia Dominic, alisema uzoefu wake wa mawasiliano, takwimu na utafiti utamwezesha kuandaa ajenda mbalimbali zitakazosaidia kuiwakilisha Tanzania kwenye masuala mbalimbali.

Katika kinyang'anyiro hicho wagombea watatu walipita awamu ya kwanza na idadi ya kura kwenye mabano ni Gladness Salame (61), Lucia Pande (49), Queenelizabeth Makune (44) ambao walikwenda hatua ya pili na kutakiwa kuchaguliwa mgombea mmoja.

Katika hatua ya pili mshindi ni Gladness aliibuka mshindi kwa kura (139) akifuatiwa na Lucia (53) na Queenelizabeth (52).

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilipokea majina ya wagombea 47 wakiomba ridhaa ya kuwania nafasi ya Ubunge wa EALA ambapo baada ya mchakato waliwateua 10 kuwania nafasi hiyo.

Nafasi hiyo ya EALA ilitangazwa baada ya kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Bunge hilo, Dk. Shongo Sedoyeka kufariki dunia Juni 13, mwaka huu.

Baada ya kumpata mgombea wa nafasi ya EALA, Septemba 5, mwaka huu, wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watapiga kura kumpitisha mbunge huyo.




Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, akizungumza na viongozi mbalimbali wa chama na serikali, wadau wa maendeleo na wananchi waliofika katika ufunguzi wa kongamano la ukusanyaji wa maoni ya wadau kuhusu Dira ya Taifa 2050 katika ukumbi wa Mikutano wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Tunguu jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafafanua sababu kupinga kesi TAMISEMI

**Na Grace Gurisha**

SERIKALI imefafanua sababu za kupinga kesi ya kuzuia Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, huku ikidai kuwa maombi yaliyowasilishwa mahakamani hayana mashiko kisheria.

Aidha, imedai kuwa maombi yaliwasilishwa na Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, Bubelwa Kaiza na Annanilea Nkya wanataka Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ndio isimamie yamekiuka Kanuni ya 5 (2)(d) ya Maboresho ya Sheria na Masharti Mbalimbali.

Ufafanuzi huo na pingamizi manne yalitolewa jana mbele ya Jaji Wilfred Dyansobera wa Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam na Wakili wa Serikali Mkuu kutoka ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Marck Mulwambo, Erigi Rumisha na Ayubu Sanga.

Wakili Sanga alidai kuwa sio kila jambo linapaswa kuwa sehemu ya kiapo, yanayotakiwa kuwapo ni yanayotakiwa pekee na kanuni hiyo inatoa matakwa ya namna ya kuwasilisha kibali cha kuomba mapitio ya kimahakama (Judicial Review).

"Ukisoma kanuni husika inatoa tafsiri mbili ambazo ndiyo msimamo wa sheria, kiapo hicho hakijiondoi kwenye matakwa yake kwa sababu kinapaswa kuwa kama viapo vya kawaida, kwa hiyo kuna mambo yanayotakiwa kuwapo na yasiyotakiwa," alidai Sanga.

Alisema ili kuunga mkono hoja hiyo aliwasilisha mahakamani hapo kesi mbalimbali za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ambazo zilikutana na mazingira ya kiapo ambacho kimejumuisha mambo ambayo hayatakiwi.

"Katika kiapo hiki cha waleta maombi kimekiuka kanuni hii kwa sababu para ya saba, tisa, kumi, 11, 12, 15,17, 18 na 19 wametoa mawazo yao na hitisho kinyume na matakwa yaliyotolewa kwenye GN 324/2004."

"Tunaomba mahakama iziondoe para hizi na ni maoni yetu hizo zilizobaki zitakuwa hazina uzito, kwa hiyo tunaomba maombi hayo yaondolewe," alidai Wakili Sanga. Alidai kuwa katika pingamizi la tatu na la nne anayajibu kwa pamoja, alidai lengo la kiapo kwenye maombi ni kubadilisha jambo kuwa kwenye ushahidi, kinachokuwapo kwenye maelezo ya waleta maombi lazima kiwapo kwenye kiapo.

"Hii inamaanisha kwamba kama kuna vitu vipo kwenye maelezo ya waleta maombi na havipo kwenye hati ya kiapo, mahakama haiwezi kuvifanyia kazi kwa sababu havipo kwenye ushahidi, kwa hiyo aliomba kuanzia paragrafu ya pili hadi 17 ziliondolewe," alidai Wakili Sanga.

Naye Wakili Rumisha aliiomba mahakama itupilie mbali maombi hayo kutokana na upungufu wa kisheria yaliyojitokeza na pia katiba na sheria vimebaina bayana kuhusiana na utaratibu huo.

Mulwambo aliiomba mahakama itupilie mbali maombi hayo kwa sababu hayana miguu ya kisheria ya kusimamia na ikiona inafaa inayatupe kwa gharama huku akidai kuwa mengi yameshaelezwa na mawakili wengine.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa waleta maombi Mpare Mpoki na Jebra Kambole, walidai kuwa mawakili hao wamejielekeza vibaya kwa sababu hakuna sheria iliyoelekeza mambo ambayo wao wameyapinga katika kiapo cha wateja wao.

Mpoki alidai wanachoomba ni mahakama kutoa kibali, kwa sababu wanachohoji ni uhalali wa TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo, wanaomba kibali cha kuzia hilo lifanywe na ofisi hiyo.

Alidai, walichodai ni kinyume na sheria ya TAMISEMI kusimamia uchaguzi huo, Katiba pamoja na sheria hawajavigusa, wanahoji uhalali, huku akidai kuwa hajui mawakili hao wana lengo gani la kupinga kibali hicho kutolewa na mahakama.

Pia, alidai kuwa hakuna sheria ya viapo waliyoitoa ambayo inakataza kutoa maoni kwenye kiapo na kudai kuwa hata hizo para ziliondolewa haziwezi kufuta mambo yao.

Wakili Jebra Kambole alidai kuwa mawakili hao walieleza baadhi ya para zina shida, lakini para 9,11,18 na 19 hawajazielezea kabisa kwa maana hiyo hazina shida na wao wanaamini para zote zipo sawa.

"Maombi yamekidhi vigezo vyote vya kwenye kanuni na vimeendana na matakwa ya sheria, haya watuambie ni kanuni ipi inalazimisha facts wanazozitaka wao. Maelezo yetu tuliyoyafaili hakuna jambo jipya kama wanavyodai wao," alidai Kambole.

Alidai kuwa maelezo (statement) sio ushahidi (Evidence), ushahidi upo kwenye kiapo ndio maana ina sehemu ya ukweli, kwa hiyo pingamizi zao hazina mashiko ya kisheria.

Kesi imeahirishwa hadi leo saa nne asubuhi kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa. Kesi hiyo imefunguliwa dhidi ya TAMISEMI na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

## MATANGAZO

# NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTILINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| UKONGA | WAWA COMPANY LIMITED | 1.NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.KND/KGG/KATI/214 KIGOGO KATI 2. NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOPO KINZUDI GOBA | 1.SALUM JUMA MARWA 2.SALUMU JUMA NYANDOTO | 1.KIGOGO KATI 2.KINZUDI GOBA | 13/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | NEZAK INVESTMENT LTD | NYUMBA YENYE HATI NA. DSMT1019002 KIWANJA NAMBA P23439 KIFURU-KINYEREZI | ZACHARIA ANTHONY KAPAMA | KIFURU KINYEREZI-ILALA | 10/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | TEMSO ENGINEERING AND CONSTRUCTION CO. LTD | NYUMBA YENYE HATI NA.58326,KIWANJA NA.2000,KITALU 'A' | RAYMOND LUDOVICK TENGA | PUGU KAJIUNGENI | 17/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KARIAKOO | MBM MOTORCYCLE SPARES | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NAMBA 101, KITALU "47", HATI NAMBA 52425 | PETER SIMON MSANZYA | KIJITONYAMA -DAR ES SALAAM | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HAJI HARAMBE BIBOZE | NYUMBA | HAJI HARAMBE BIBOZE | VIKINDU MASHARIKI | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | NYUMBA (2) ZENYE HATI MILIKI | KIVAULA MLIMKA LUHANGA | 1.SABA SABA MBEYA MJINI 2. TUNDUMA | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | PRIVA EMANUEL SHIRIMA | KITETE-MBEYA | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | BAHATI YOHANA NYATO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | BAHATI YOHANA NYATO | LYAMKENA-MAKAMBAKO | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | FRENK SAMSON LEMAU | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | FRENK SAMSON LEMAU | SHEWA-MBEYA | 13/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | IPYANA TIGER JUNIOR | NYUMBA | IPYANA TIGER JUNIOR | ILEMI | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | HELENA ANTONY HALENGO | NYUMBA | MARIA ANTHONI SKAWEWE | ILEMI | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| DODOMA | CHARLES SIMON MALOMELE | NYUMBA | CHARLES SIMON MALOMELE | NDACHI-DODOMA | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | JONATHAN ZAWADI MHANDO | NYUMBA | JONATHAN ZAWADI MHANDO | MBEZI- MSAKUZI | 06/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KARIAKOO | LAMECK JOHN RUGIGA | NYUMBA | LAMECK JOHN RUGIGA | KIBAMBA MBEZI | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | LATIFA MOSHI MLANZI | NYUMBA | SALUMU OMARI AMIRI | MWANDEGE - MKURANGA | 23/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | OSCAR ELIAMINI CHUWA | NYUMBA | FLORA ELIAMINI CHUWA | MBAGALA KIZUIANI | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | HOSEA MARCO OOKO | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | DAUDI JAKAMUGAH MAKOSIGAH | NYUMBA | KIBADENI J. NYATIENO | ZAVARA -ILALA | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | ATUPELE LABAN MWAIJIBE | NYUMBA | DR. ATUPELE LABAN MWAIJIBE | KIPUNGUNI | 09/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | FELIX BIRCKMAS ALOYS | NYUMBA | KASSIAN ANTHON NINDI | TABATA KISUKULU | 24/09/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 13/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | NELSON JUDICA KIMARO | NYUMBA (2) | 1.NELSON JUDICA KIMARO 2.ERICK ISHENGOMA BILIKWIJA | 1.KIMARA BONYOKWA 2.MABIBO | 19/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | FATUMA HAMISI SONGORO COSTANTINO JO | NYUMBA | FATUMA HAMISI SONGORO | BAGAMOYO-UKUNI | 20/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| DODOMA | KOLE JOSEPH SAINI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KOLE JOSEPH SAINI | BOMBAMBILI ILALA DAR ES SALAAM | 23/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JESCA PETER SHIRIMA | NYUMBA | JESCA PETER SHIRIMA | MJOHORONI MOSHI | 20/08//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | CHEGE REUBEN OGILLO | NYUMBA | CHEGE REUBEN OGILLO | MSARANGA MOSHI | 13/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | NYUMBA | MWAJABU AHMEDI KIBWANA | BOMANG'OMBE HAI | 13/09/2024 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | JUMA SELEMANI MNDEME | NYUMBA | JUMA SELEMANI MNDEME | MWANGA | 23/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | PLUKERIA MARTIN MANINGI | NYUMBA | PLUKERIA MARTIN MANINGI | KIBOSHO -KOMBO | 26/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SAMIJI ATHUMANI KIMBWEREZA | MAKANYA SAME | 15/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | MOSES YARED CRY | NYUMBA | MOSES YARED CRY | ZAVARA BUYUNI | 06/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | BARAKA NELSON NYIRENDA | PAGALE LA NYUMBA | BARAKA NELSON NYIRENDA | BUNJU 'B' | 19/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | VENANCE CLEMENCE NYARI | NYUMBA | VENANCE CLEMENCE NYARI | TEGETA WAZO | 17/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | ANNA IVAN SUTILA | NYUMBA | ANNA IVAN SUTILA | MBEZI JUU | 17/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | JOSEPH DASTAN BARUA | NYUMBA | JOSEPH DASTAN BARUA | SARANGA | 18/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | RAYMOND SAMSON LAISER | NYUMBA | RAYMOND SAMSON LAISER | KIHARAKA BAGAMOYO | 19/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | NYUMBA | LAURENCIA ROBERT KIROBI | KIBADA | 17/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | DANIEL FADHIL MINJA | NYUMBA | DANIEL FADHIL MINJA | MAJOHE | 18/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | NYUMBA | RENIFRIDA CHARLES MGUDE | SARANGA | 19/09//2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MICHAEL HAYSHI QAMARA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI KIWANJA NA. 58 KITALU ' C ' | MICHAEL HAYSHI QAMARA | KARATU | 23/09//2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | HEALSUN PRE & PRIMARY SCHOOL | NYUMBA | LILIAN PHILEMON LAIZER &EDWARD N. LAIZER | SEKEI-ARUSHA | 26/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | FRANK RUBEN AKYOO | NYUMBA | FRANK RUBEN AKYOO | NKOARISAMBU-ARUMERU | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | RABSON NICHOLOUS SWAI | NYUMBA | RABSON N. SWAI | LEGURUKI-MERU | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | OLIVER STANLEY MNDEME | NYUMBA | OLIVER STANLEY MNDEME | KIMANDOLU - ARUSHA | 25/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | EMMANUEL LEJASA KIMATH | NYUMBA | EMMANUEL LEJASA KIMATI | SINONI -ARUSHA | 24/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | SIMON ANAEL SARAKIKYA | NYUMBA | SIMON ANAEL SARAKIKYA | NKOANRUA-ARUSHA | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LUCY FLORIAN TESHA | NYUMBA | LUCY F. TESHA | MOSHONO - ARUSHA | 26/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | LIGHTNESS JOSEPH MONGI | NYUMBA | LIGHTNESS JOSEPH MONGI | MURIETH -ARUSHA | 25/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ELIMULICA MESIAKI MOLLEL | NYUMBA | REGAN MESIAKI MOLLEL | MOIVO -ARUSHA | 27/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | MSAFIRI LONING'O SAYAREN | NYUMBA | MSAFIRI LONING'O SAYAREN | MOSHONO KASKAZINI - ARUSHA | 17/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ARUSHA | ELISANTE ERASTO KINANDE | NYUMBA | ELISANTE ERASTO KINANDE | MURIETH -ARUSHA | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MARIA JOHN PETRO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOHN PETRO KALISA | KILOLELI 'B' - MWANZA | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYASAKA | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | GRACE ADONIAS MTEGO | NYUMBA ILIYOPO KWENYE KIWANJA NA.22 KITALU 'N' HATI NA.4870 | BLASIUS SWAI KAGINA | BUNDA | 21/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MWANZA | ABAS HAMAD ISSA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PETER NDULU MAHARAGE | MISUNGWI | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JAMES JACOB KALULEMA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JAMES JACOB KALULEMA | NYANGURUGURU MAHINA | 22/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | KITU MAYALA MANGA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | KITU MAYALA MANGA | KISESA | 26/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MAWAZO JOHN SIMON | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | EDWIN GASPARY NYAMTABA | KANYERERE | 23/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JOSIAH JOHN JOACHIM | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | JOSIAH JOHN JOACHIM | KISESA MWANZA | 23/09/204 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | NICHOLAUS PIUS HEZWA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | NICHOLAUS PIUS HEZWA | NYASAKA ILEMELA | 21/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | LEVINA FELIX RWEBANGIRA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | PAUL EUSTARD RWEYEMAMU | MJI MWEMA MWANZA | 21/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | JUMANNE MOHAMED KAPOLI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | MATHIAS CHARLES NDETTO | KISESA MWANZA | 26/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | CHACHA ITEMBE NYAMAISA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SHABANI S. BULILO | NYAMHONGOLO | 27/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | HELENA IGNATUS NYAKARASHI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | GEORGE SILIVESTER ADOGO | NYAMADOKE BUSWERU | 22/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SIKITU HAMIS YAHAYA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | HAJI ABEID KASUBI | NYASAKA | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | SELEMANI CHARLES MNIKO | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | SELEMANI CHARLES MNIKO | MBUGANI -MWANZA | 15/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | NYUMBA | ABDILLAHI SAIDI KANYWANYI | YOMBO VITUKA | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | BUNDALA SOSELA NDUNGUMIKA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI | BUNDALA SOSELA NDUNGUMIKA | BUYUNI-CHANIKA | 17/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | NYUMBA | ABDALLAH AHMAD MUHIDINI | TEGETA 'A' - GOBA | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | NYUMBA | MARTHA ONESPHORY NCHIMBI | MGEULE JUU-CHANIKA | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BRILUCK SECRETARIAL SERVICE | NYUMBA | ADOLF ANSELM MNG'ANYA | MBEZI MSAKUZI | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MICHAEL LAURENTI MPOGOLE | NYUMBA | MICHAEL LAURENTI MPOGOLE | MBEZI KIBAMBA | 20/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | SALUM RAJABU MCHOMVU | NYUMBA | SALUM RAJABU MCHOMVU | MAJOHE | 11/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEMEKE | AMRI BAKARI MAKANYA | NYUMBA | MWANAHAMISI KASSIM YUSUPH | KITUNDA | 09/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TANDALE | JUMA ALLY NGAWANAE | NYUMBA | JUMA ALLY NGAWANAE | MABWEPANDE | 12/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | KURUTHUMU ALLY HUSSEIN | NYUMBA | FUAD JAFARI ABDALLAH BIN SHMLAN | PEMBA MNAZI -KIGAMBONI | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | JACQUELINE LAMECK KIBOGA | NYUMBA | SABATO DAVID OKUKU | MIKWAMBE- TOANGOMA | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UBUNGO | CESILIA SAMWELY KWEKA | NYUMBA | LEONARD JACOB NUBWA | MBAGALA- MISSION | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | MTUMWA SALUM HAMAD | NYUMBA | MATONGO NKWABI NSWAGA | PUGU KINYAMWEZI | 17/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ANDREW SAMSON GESURURA | NYUMBA | ANDREW SAMSON GESURURA | BASIHAYA-BOKO | 12/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | MUSSA INANO CHACHA | NYUMBA | HABIBU MUSSA MACHOROKO | MBAGALA | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | SAINT PIO DAY CARE CENTRE | NYUMBA | JESCA JAMES SUGWEJO | MABWEPANDE | 17/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | KOKUBELWA PAUL NGAMBEKI | KIWANJA | ANTHONY AARON ICHWEKELEZA | MPIJI MAGOE | 16/09/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| AGGREY | MWANAHAMIS VITUS FRANK | NYUMBA | HADIJA MOHAMED CHANDE | MSINGWA-MSIGANI | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SELEMANI HEMED SELEMANI | NYUMBA | SELEMANI HEMED SELEMANI | MBAGALA KIBONDE MAJI | 17/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SHAMSI FADHILI MASISA | NYUMBA | SAAD ADAM MDOE | KINYAMWEZI KATA YA PUGU | 19/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | WINNIE ADOLE RWIZA | NYUMBA | WINNIE ADOLE RWIZA | KANGA-KINYEREZI | 18/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SALVATORY MODESTI NGOWI | NYUMBA | SALVATORY MODESTI NGOWI | KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 16/09/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0714939933/0759648448/0715868000/0714208208/0759648448/0755337777/0715363537/0713306054
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FILEXY CHAMY** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya King Lion yenye namba za usajili **MC 281 DAZ,** Chasis namba ***LZL15P904MHH42889*** na Engine namba **KL162FMJ*210842889*.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/MAN/BAB/2657/2023.**

## KUPOTEA KWA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

**ESTER ALEX MGEMO** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja namba **401 kitalu "jj"** ndembezi manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya polisi
**PHQ/SHI/SHI/7577/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**RASHID HALIDI,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya boxer yenye namba za usajili **MC 250 DDG.** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/20661/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FATUMA ISSA SALUM,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya boxer 150 yenye namba za usajili **MC 764 CCY.** Engine no **pfzwjc92822,** Chassis no **Mdza21by8jwh88058,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
TAARIFA YA POLISI:
**PHQ/DOD/DOD/34497/2024**

HABARI KITAIFA/KIMATAIFA

# TARURA kutumia bil. 1.2/ ujenzi barabara, masoko halmashauri 6

Na Elizabeth Zaya

WAKALA wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), imetangaza kuanza awamu ya pili ya mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP), utakaogharimu Dola za Marekani milioni 438 (bilioni 1.2).

Mradi huo utahusisha halmashauri tano za jiji hilo kwa kipindi cha miaka sita, barabara zitakazojengwa ni zenye urefu wa kilomita 250, mifereji ya kilomita 90, vituo vya mabasi tisa, masoko 18, madampo matatu na kuwanufaisha wananchi milioni 3.8.

Kwa mujibu wa TARURA, utekelezaji wa mradi huo upo katika hatua ya ukamilishaji wa ununuzi wa makandarasi na kuanza rasmi ujenzi huo.

Kadhalika, wakala huo umesema umepanga kuanza mradi wa uboreshaji wa miundombinu kwa kuhusisha ushindani katika majiji matano nchini, manispaa 16 na miji 24.

Katika miji 12 ya kwanza utekelezaji umeanza wa ujenzi wa barabara na mifereji ya maji ya mvua ambayo mikataba yake ilisainiwa Septemba 23, mwaka jana na utachukua muda wa miezi 15.

Mtendaji Mkuu wa TARURA, Victor Seff, alisema hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, barabara zenye kiwango cha changarawe za wilaya zilikuwa zimefikia kilomita 42,059.17 huku barabara za lami za wilaya zikifikia kilomita 3,337.66.

kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja na uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi, Seff alisema kaya nyingine 314 zinatarajiwa kuathirika na mradi huo na tayari mchakato wa kuandaa daftari la fidia kulipa kaya hizo utaanza mwezi huu.

Alisema ununuzi wa mkandarasi atakayejenga daraja katika eneo hilo la Mto Msimbazi pamoja na mhandisi msimamizi wake unatarajiwa kukamilika Novemba, mwaka huu.

"Lengo la mradi ni kukabiliana na mafuriko katika Bonde la Mto Msimbazi ambapo eneo la chini la mto huo linatarajiwa kuongezewa kina na kupanuliwa ili kuruhusu maji kwenda baharini kwa kasi inayotakiwa.

Kuhusu mafanikio waliyofikia kwa kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa mpango mkakati wa mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2023/2024, alisema kazi zilizofanyika kwa kipindi hicho ni ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 923.96, barabara za changarawe kilomita 22,815.98 na madaraja 378.

Pia, alielezea hali ya mtandao wa barabara za wilaya kufikia Juni, mwaka huu asilimia 36.52 zilikuwa na hali mbaya, asilimia 35.26 hali ya wastani na ambazo zilikuwa nzuri kipindi hicho ni asilimia 28.22 na kwamba sababu kubwa ya uharibifu ilikuwa ni mvua ambazo zilichangia nyingine kushindwa kupitika.

Alisema lengo la TARURA ni kuhakikisha inaboresha zaidi miundombinu ya barabara hizo ili zipitike katika vipindi vyote bila kukwamisha shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Alisema mpango mkakati wa pili wa TARURA wa mwaka 2021/22 hadi mwaka 2025/026 umeanza kutekelezwa tangu mwaka 2021 ambao kufikia sasa utekelezaji wake umefikia asilimia 50 ya malengo.

Kuhusu utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa barabara za vijijini na fursa za kiuchumi na kijamii unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Tanzania, Seff alisema unatarajiwa kugharimu Sh. bilioni 822.5 na kwamba Sh. bilioni 705 ni mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia na Sh. bilioni 117.5 ni mchango wa serikali.

Alisema mradi huo unatarajiwa kujenga Kilomita 533 za lami ambapo kilomita 400 ni za TARURA na 135 ni za Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) na utekelezaji wake umeanza katika mkoa wa Iringa kilomita 33 za Wenda hadi Mgama, Kilomita 19 na Mtilili hadi Ifwagi, na Kilomita 14 zilizopo kwenye halmashauri za wilaya ya Iringa na Mufindi.

Pia, alisema usanifu wa barabara za kilomita 50 za mwanzo kwa kila halmashauri kupitia mradi huo, Ruangwa, Mbogwe na Handeni umefikia asilimia 75.



Mhudumu wa afya akichukua vipimo kwa washukiwa wa homa ya nyani nchini Uganda. **PICHA: MTANDAO**

# Wananchi waandamana Israel kushinikiza mateka kuachiwa

**JERUSALEM, Israel**

MAELFU ya watu wamekusanyika nchini Israel baada ya miili sita ya mateka wa Hamas katika Ukanda wa Gaza kupatikana na wanajeshi wa taifa hilo, na kusababisha ghadhabu ya kitaifa na kusababisha maandamano ili kushinikisha mchakato wa makubaliano ya kuachiwa mateka.

Ilielezwa jana kuwa waandamanaji, wengi wakiwa wamevaa bendera za Israel walishuka Tel Aviv, Jerusalem na miji mingine, wakimtuhumu Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu na serikali yake kwa kutofanya vya kutosha kufikia makubaliano ya kuachiliwa kwa mateka waliobaki chini ya Hamas.

Maandamano hayo yaliyoanza Jumapili yalielezwa kuwa kwa kiasi kikubwa yalikuwa ya amani, lakini umati wa watu ulivunja vizuizi vya polisi, na kuziba barabara kuu ya Tel Aviv, kama sehemu ya kushinikiza mamlaka kufanyia kazi hitaji lao.

Pia ilibainishwa kuwa haya yanajiri wakati chama kikuu cha wafanyakazi nchini Israel, Histadrut, kilipoitisha mgomo mkuu wa nchi nzima jana ili kushinikiza makubaliano kuhusu waliotekwa nyara na kundi la Hamas.

Hata hivyo, Jeshi la Ulinzi la Israel (IDF) lilisema awali kwamba miili hiyo sita ilipatikana siku ya Jumamosi kwenye handaki la chini ya ardhi katika eneo la Rafah kusini mwa Ukanda wa Gaza.

Vile vile, mateka hao walitambuliwa kuwa ni Carmel Gat, Eden Yerushalmi, Hersh Goldberg-Polin, Alexander Lobanov, Almog Sarusi na Mwalimu Sgt Ori Danino.

IDF ilisema baada ya kuipata miili hiyo walibaini kuwa wahusika walikuwa wameuawa muda mfupi kabla ya wanajeshi wa Israel kuwafikia. Na kwamba hali hiyo ilizua maandamano, huku umati wa watu wakishutumu serikali na Waziri Netanyahu kwa kushindwa kuwaokoa mateka waliosalia.

*BBC*

# Mpox yasambaa kila kona Uganda

**KAMPALA, Uganda**

WIZARA ya Afya nchini Uganda imesema kuwa ugonjwa hatari wa Homa ya Nyani (Mpox) umesambaa katika kila sehemu ya taifa hilo, huku ikisisitiza wananchi kutoa taarifa mapema wanapomwona mtu mwenye dalili hatarishi.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa ya wizara hiyo iliyotolewa jana, ikieleza kuwa mamlaka za afya sasa zimo mbioni kudhibiti kusambaa zaidi kwa ugonjwa huo huku hofu ikiwa ni kwamba ni kipindi cha likizo ya shule na watoto wamerudi.

Julai 24, mwaka huu, kisa cha kwanza cha ugonjwa wa Mpox kiliripotiwa kwenye mji wa Bwera Wilaya ya Kasese Mpakani na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC).

Japokuwa Wizara ya Afya ilihakikisha kuwa ilikuwa imeweka mikakati ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo, sasa imesema kwamba ugonjwa huo umesambaa sehemu mbalimali za nchi na kwamba huenda idadi ya waathirika ikawa kubwa zaidi.

Luteni Kanali Henry Kyobe ambaye ndiye husimamia masuala ya milipuko katika wizara hiyo alithibitisha visa hivyo na kuhimiza umma kuwafichua mapema wale walio na ishara za ugonjwa huo.

Pia alitoa mwito kutowanyanyapaa waathirika kwa kuwa hali hiyo itawasababishia kujificha wasipate matibabu na kuendelea kusambaza ugonjwa huo.

"Tunafanya kila juhudi kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huo, lakini tunahimiza dhidi ya uyanyapaa kwa wagonjwa hao," alisema Kyobe.

Kwa mujibu wa wizara hiyo kuna angalau mwathirika mmoja katika kila kanda ya nchi Kaskazini, Magharibi, Mashariki na katikati mwa nchi.

Miongoni mwa kile kinachoelezewa kuchangia maambukizi ni mienendo ya ngono ya waendeshaji wa magari ya mizigo. Na kwamba dereva mmoja wa Kenya aliyegunduliwa kuwa na ugonjwa huo nchini kwao alikuwa ametokea Uganda akielekea Rwanda kupitia nchi hiyo.

Ofisa Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) mjini Kampala, Dk. Annet Alenyo, alisema ishara ya ugonjwa huo hudhihirika kwa awamu tatu, ikiwamo kuumwa na kichwa, udhaifu na homa mwilini, kuwashwa koo. Na awamu ya pili ni pale vipele vinapojitokeza na kusambaa mwili mzima.

Pia ilielezwa kuwa siku chache zilizopita wanakijiji huko Busia walikumbana na ishara hizo baada ya mtu mmoja kufariki na hadi sasa wanahofia kuwa ni Homa ya Nyani.

*DW*

# NDONDO CUP YASAIDIA VIJANA KUPATA HUDUMA VVU, CHANJO

**Na Mwandishi Wetu**

MICHUANO ya Ndondo Cup, mwaka huu imechukua sura mpya kutoka kuwa mashindano ya mpira wa miguu hadi tukio muhimu la uhamasishaji na utoaji wa huduma za afya kwa jamii.

Utoaji wa huduma za afya ulimwezeshwa kwa juhudi za pamoja za Serikali ya Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), na mradi wake wa Breakthrough ACTION, Mfuko wa Dharura wa Raisi wa Marekani wa Kupambana na Ukimwi (PEPFAR), pamoja na Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mpango huu pia umehusisha ushirikiano wa karibu na waandaaji na wadhamini wengine wa Ndondo Cup. Ushirikiano huu umewawezesha vijana wa kiume na wavulana kuendelea kupata huduma muhimu za VVU na chanjo huku wakishangilia timu zao pendwa.

Kuwashirikisha vijana wa kiume wenye umri wa miaka 15-24 katika huduma za afya - hasa upimaji wa VVU na kinga - imekuwa ni changamoto kwa muda mrefu sasa. Kwa kuliona hitaji hili, Breakthrough ACTION ilitambua Ndondo Cup kama jukwaa bora na muhimu la kufikia kundi hili katika mazingira ambayo wanapatikana na kufikiwa kwa urahisi.

Mkurugenzi wa Mradi wa Breakthrough ACTION nchini Tanzania, Waziri Nyoni, akizungumzia michuano hiyo mwishoni mwa wiki, alisema, ufanisi wa mashindano ya Ndondo Cup unaonesha umuhimu wa ushirikiano katika kuboresha afya ya umma.

Nyoni aliongeza: „Juhudi za pamoja kati ya Tanzania na Serikali ya Marekani kupitia wadau wake Breakthrough ACTION, MDH na EpiC katika kuhamasisha na kutoa huduma za afya hasa za VVU na chanjo, zimekuwa muhimu katika kuondoa vikwazo vya upatikanaji wa huduma za afya hasa kwa wanaume na vijana.“

Katika mashindano yaliyofanyika Dar es Salaam, huduma za upimaji wa VVU na chanjo zilitolewa kwa kushirikiana na MDH na EpiC wadau wa afya waliohakikisha kwamba huduma hizi muhimu zinafikishwa kwa urahisi na kwa siri.

Mpango huu ulijumuisha msisimko wa michezo na mijadala muhimu kuhusu VVU na chanjo, na hivyo kuleta pamoja juhudi za kitaifa na za kijamii za kuboresha afya.

Wakati wa mashindano hayo, ambayo yalihudhuriwa na zaidi ya watu 70,000, takriban vijana 10,000 walipatiwa huduma za upimaji wa VVU na chanjo. Aidha, juhudi za uhamasishaji nchi nzima zilifikia zaidi ya watu milioni 13 kupitia majadiliano katika redio na mitandao ya kijamii yaliyolenga kuongeza uelewa kuhusu VVU na chanjo.

Ndondo Cup imeonesha jinsi matukio ya michezo yanavyoweza kutumika kama kichocheo chenye nguvu cha kuhamasisha afya na ustawi, na hivyo kuweka kiwango kipya cha kuboresha afya ya umma kupitia ushirikishwaji wa jamii.




Wawakilishi wa udhamini wa michuano ya Ndondo Cup 2024, wakiwa tayari kutoa medali kwa washindi mbalimbali wa fainali hizo ambazo zilichezwa jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wakati wa mashindano hayo, vijana 10,000 walifaidika na huduma za afya ikiwamo kupima VVU na chanjo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## EATV miongoni mwa wadhamini mbio za mbuzi 2024

**Na Mwandishi Wetu**

TAMASHA la mbio za Mbuzi lililoandaliwa na Klabu ya Rotary Oysterbay, linatarajia kufanyika Septemba 21, mwaka huu, kwa lengo la kukusanya Sh. milioni 400 za kusomesha wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Rais wa Klabu ya Rotary Oysterbay, Himanshu Bhattbhatt, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tamasha hilo, lililodhaminiwa na kampuni 19 ikiwamo ya Simu ya Vodacom, Kituo cha Luninga cha EATV na East Afrika Redio.

Alisema tamasha hilo linalotarajia kuhusisha washiriki 4,000, litafanyika kwa mara ya saba tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018, kwa lengo la kushirikiana na serikali kuboresha sekta ya elimu nchini.

"Mbio za Mbuzi mwaka huu zitafanyika Septemba 21 na leo (jana) tupo hapa kutangaza wadhamini wetu waliojitokeza kutuunga mkono kufanikisha mbio hizi zenye lengo la kusaidia jamii moja kwa moja," alisema.

Tamasha hilo linatarajiwa kufanyika katika viwanja vya The Green Oysterbay jijini Dar es Salaam kuanzia saa 6:00 mchana hadi saa 2:00 usiku.

Alisema kupitia tamasha hilo, washiriki ambao ni watu wazima na watoto watapata burudani mbalimbali kupitia michezo iliyoandaliwa na washindi watapatiwa zawadi mbalimbali.

Mwakilishi wa EATV, Mariam Shabani, alisema wameguswa kudhamini mashindano hayo kwa sababu yanagusa jamii moja kwa moja.

Naye Mkuu wa Uhusiano kwa Umma na Vyombo vya Habari wa Vodacom, Annette Kanora, alisema wamevutiwa kuendelea kuwa wadhamini kwa sababu wameshuhudia jamii ikinufaika.

"Baada ya kuona mafanikio yaliyotokana na mbio za mbuzi za mwaka 2023, kampuni imevutiwa kuendelea kudhamini mbio hizi za hisani kwa mwaka wa pili mfululizo," alisema Annette.

Mwakilishi wa Kampuni ya The Tanzanite Dreems inayojihusisha na vito vya thamani, Shadya Latiff, alisema wanaona kuna haja ya kugusa jamii yenye uhitaji hususan sekta ya elimu.

Mbio za mwaka jana zilikusanya Sh. milioni 340 ambazo zilitumika kusaidia wanafunzi wa vyuo vikuu wenye uhitaji katika kufanikisha malengo yao ya kupata elimu.

Fedha hizo zinatumika katika kuboresha mazingira ya elimu, kutoa ufadhili wa elimu kwa wanafunzi wenye uhitaji na kuimarisha miundombinu ya maji na usafi shuleni.

## 'Sarakasi' za maamuzi zaibuka Namungo

**Na Faustine Feliciane**

VIPIGO viwili mfululizo kwenye michezo ya Ligi Kuu vimeibua sarakasi za maamuzi kwenye uongozi wa klabu hiyo kuhusu uhai wa benchi la ufundi la timu hiyo.

Wakati mapema jana, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, akisema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera, ameondolewa kwenye nafasi hiyo kutokana na matokeo mabaya waliyoyapata kwenye michezo miwili, muda mfupi baadaye kiongozi mwingine wa Namungo alitoa taarifa ya kumwongeza kwenye benchi la ufundi, Kocha Ngawina Ngawina, kushirikiana na Zahera na wengine kukinoa kikosi hicho.

Mwenyekiti Zidadu, mapema alithibitisha kuachana na kocha huyo kutokana na matokeo hayo mabaya, lakini klabu ilikanusha na kutoa taarifa ya Zahera kuendelea kuwa kocha mkuu wa timu hiyo akisaidiwa na Ngawina, Shadrack Nsajigwa na Vladimir Niyonkuru.

"Uongozi wa Namungo unapenda kutaarifu umma kuwa umeongeza nguvu kwenye benchi la ufundi kwa kumleta Kocha Msaidizi Ngawina Ngawina, kocha mkuu ataendelea kuwa Mwinyi Zahera," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Awali, kabla ya taarifa hiyo ya klabu, Kocha Zahera aliiambia Nipashe kuwa yeye bado ni kocha wa timu hiyo kwa kuwa hakuna taarifa rasmi ya tofauti aliyopewa na viongozi wake.

"Mimi bado kocha wa Namungo, hatujapata matokeo mazuri kweli katika mechi zetu mbili, yapo mambo yaliyojitokeza kiufundi uwanjani na tunayafanyia kazi," alisema Zahera.

Namungo imejikuta ikipoteza michezo miwili mfululizo wakiwa nyumbani kwa kukubali vipigo kutoka kwa Tabora United (1-0) na Fountain Gate (2-0).

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL NA OSIMHEN

LIVERPOOL ilichunguza uwezekano wa kumsajili mchezaji wa Kimataifa wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 25, katika dirisha la usajili la kiangazi, lakini wakakatishwa tamaa na mshahara mkubwa wa fowadi huyo wa Napoli. ***(Corriere dello Sport)***

### TRIPPIER KUELEKEA SAUDIA

MLINZi wa kulia wa Newcastle, Kieran Trippier huenda akaelekea katika moja ya klabu zinazovutiwa naye nchini Saudi Arabia, huku beki huyo wa zamani wa England mwenye umri wa miaka 33, akitaka kuondoka katika klabu hiyo ya Kaskazini Mashariki. ***(Sun).***

### NEWCASTLE YAKANUSHA

KLABU ya Newcastle United imepuuza mapendekezo kwamba Kieran Trippier anataka kuondoka katika klabu hiyo na kuhamia Saudi Arabia au Uturuki. ***(Sportsport)***

### WILLIAN AENDA UGIRIKI

WINGA wa zamani wa Chelsea na Fulham, Willian mwenye umri wa miaka 36, amesafiri kwa ndege hadi Athens huku Olympiakos wakiwa na nia ya kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil. ***(Fabrizio Romano)***

### DEPAY NA SEVILLA

SEVILLA inaonekana kupunguziwa bei ya kumnunua fowadi wa Uholanzi, Memphis Depay mwenye umri wa miaka 30, ambaye anavutia Ulaya baada ya kuondoka Atletico Madrid***. (Marca)***

### HUMMELS AWANIWA ROMA

AS Roma pia ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa kati wa zamani wa Ujerumani na Borussia Dortmund, Mats Hummels mwenye umri wa miaka 35, huku wakitafuta kuchukua nafasi ya beki wa zamani wa England, Chris Smalling mwenye miaka 34, ambaye anaelekea katika Klabu ya Saudi Pro League, Al-Fayha. ***(Sky Sports Italia)***

### TONEY MSHAHARA JUU

MSHAMBULIAII wa England, Van Toney mwenye umri wa miaka 28, atalipwa pauni 403,000 baada ya kuhamia Al-Ahli, kutoka Brentford. ***(Mirror)***

### LEWIS KUTUA SAO PAULO

BEKI wa Newcastle United na Ireland Kaskazini, Jamal Lewis mwenye umri wa miaka 26, anakaribia kuhamia Klabu ya Brazil ya Sao Paulo. ***(Belfast Telegraph)***

### HERMOS HUYOOO ROMA

KLABU ya AS Roma inakaribia kumnunua mlinzi wa Hispania Mario Hermos mwenye umri wa miaka 29, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Atletico Madrid msimu wa majira ya joto. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### HARRIS KWENYE RADA

FOWADI wa Oxford, Mark Harris mwenye umri wa miaka 25, bado yuko kwenye rada za timu mpya katika ligi ya Bundesliga, Holstein Kiel, ambayo ilijaribu kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Wales msimu huu wa majira ya kiangazi. ***(Sun)***

## DONDO OKA MAGAZE LAYA




# SALAH: MSIMU HUU WA MWISHO KWANGU LIVER

●●● Nahisi niko huru kucheza soka na tutaona kitakachotokea mwaka ujao, hakuna mtu...

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI Mohamed Salah amesema huu unaweza kuwa msimu wake wa mwisho kwa Liverpool kwani mkataba wake unamalizika mwishoni mwa kampeni hii.

Salah mwenye umri wa miaka 32, alizungumza baada ya ushindi wa mabao 3-0 wa Liverpool wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford ambapo alifunga bao moja na pia kutoa pasi mbili za mabao.

„Nilikuwa na majira ya joto mazuri; nilikuwa na muda mrefu wa kukaa mimi mwenyewe na kufikiria vema, kama unavyojua ni mwaka wangu wa mwisho katika klabu," alisema Salah akiiambia Sky Sports.

"Nataka tu kufurahia. Sitaki kufikiria juu ya hilo - nahisi niko huru kucheza soka na tutaona kitakachotokea mwaka ujao.

"Hakuna mtu katika klabu ambaye amezungumza nami kuhusu mkataba, kwa hivyo ni sawa nitacheza msimu wangu wa mwisho na tutaona mwishoni mwa msimu. Si juu yangu."

Liverpool ilikataa ofa ya pauni milioni 150 kutoka kwa timu ya Saudi Pro League ya Al Ittihad kwa ajili ya Salah mnamo Septemba 2023 na licha ya ripoti za jaribio jipya la timu za Saudi Arabia kutaka kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Misri msimu huu wa majira ya joto, hakuna ofa thabiti iliyotolewa kwa mshambuliaji huyo.

Na ingawa mkataba wa Salah sasa uko katika mwaka wake wa mwisho, kocha wa Liverpool, Arne Slot alisema hatazungumzia hali ya mchezaji huyo.

„Kwa wakati huu Salah ni mmoja wetu na ninafurahi sana kuwa mmoja wetu," alisema Slot. „Alicheza vizuri sana, lakini sizungumzii kuhusu mikataba."

Salah ni mmoja wa nyota watatu wa Liverpool ambao wako ndani ya mwaka wa mwisho wa mikataba yao.

Nahodha wa klabu Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold pia wanatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu isipokuwa kama tu watakubaliana juu ya mkataba mpya wa kuongeza muda wao wa kukaa Anfield.

Salah
kutoa as
izoichez

HABARI MICHEZO

# MBAPPE: SIKUWA NA SHINIKIZO LA KUFUNGA




**MADRID,** HISPANIA

KYLIAN Mbappe amefunga mara mbili katika kipindi cha pili kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu - la kwanza baada ya pasi ya kisigino ya Federico Valverde, na la pili kwa mkwaju wa penalti - baada ya mechi tatu za ligi bila kufunga goli, lakini juzi akiziona nyavu dhidi ya Real Betis.

“Shinikizo nililonalo ni kuzoea timu,” alisema Mbappe, akizungumza na waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

“Nimefunga mabao katika maisha yangu yote, nitafunga mabao kwa uhakika. Mabao yatakuja. Mechi tatu bila kufunga ni nyingi kwangu, lakini ni sawa, nina imani na wachezaji wenzangu.”

Mbappe alifungua akaunti yake kwa Madrid dhidi ya Atalanta kwenye UEFA Super Cup mwezi uliopita, lakini hakufunga bao dhidi ya Real Mallorca, Real Valladolid na Las Palmas kwenye LaLiga, Madrid walipotoka sare mbili kati ya mechi tatu za kwanza za ligi.

“Hakuna shinikizo, ni mpira wa miguu,” alisema Mbappe.

“Nina ubora wangu. Nipo hapa kuwa Kylian. Hakuna shinikizo. Nina furaha, nataka kufanya kazi.”

Mbappe alipiga jumla ya mashuti tisa kwenye mchezo huo dhidi ya Betis.

“Ilikuwa wakati mzuri,” Mbappe aliiambia Real Madrid TV. “Nimekuwa nikingoja kufunga kwenye uwanja huu wa hadithi, bora zaidi ulimwenguni. Mashabiki wananipa mapenzi mengi, hata nilipokuwa sifungi.”

“Hatujawahi kuweka shinikizo kwake kufunga mabao,” alisema kocha Carlo Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa baada ya mechi.

Madrid sasa wako nafasi ya pili kwenye LaLiga, pointi nne nyuma ya vinara Barcelona, kuelekea mapumziko ya mechi za kimataifa.

## Muller aweka rekodi mpya Bayern Munich

**MUNICH,** UJERUMANI

THOMAS Muller aliweka rekodi Bayern Munich alipotoka kwenye benchi na kufunga katika ushindi wao dhidi ya Freiburg Jumapili, na bado kuna mengi zaidi kutoka kwa mchezaji huyo wa miaka 34, kwa mujibu wa kocha, Vincent Kompany.

Kuingia kwa Muller akitokea benchi kulimfanya acheze mechi ya 710 akiwa na Bayern, na kuipita rekodi iliyowekwa na kipa Sepp Maier aliyestaafu mwaka 1979, na bao lake la 150 la Bundesliga lilihitimisha ushindi wa mabao 2-0.

Katika hali ya kushangaza, mnamo 2008 Kompany alikuwa akicheza mara ya mwisho kama mchezaji nchini Ujerumani katika mechi ambayo Muller alicheza mechi yake ya kwanza, kabla ya kocha huyo wa sasa wa Bayern kuondoka Hamburg SV na kujiunga na Manchester City.

“Bora. Nilishuhudia mechi yake ya kwanza. Nilikuwa pale na Hamburg kwenye uwanja huu. Mechi 710 baadaye, hongera kwake,” alisema Kompany.

“Alitoa asilimia 100 katika michezo 710, lakini si tu katika michezo, lakini katika mazoezi. Hilo ndilo linalomfanya Thomas kuwa maalum.

“Kuna michezo mingine michache ambayo bado anaweza kucheza na bila shaka tunafurahi kwamba ana mingine michache kwenye kabati lake na ukweli kwamba anaweza kuendelea hivi, ni muhimu sana kwetu.”

Kompany alisema kiwango cha timu yake kilishuka baada ya mapumziko, lakini kwa bahati nzuri ana wachezaji kama Muller ambao anaweza kuwaita pindi inapohitajika.

“Kipindi cha kwanza kilikuwa chanya sana, halafu kipindi cha pili tulikuwa hatua moja tu baadaye kuliko Freiburg kwenye mipira ya pili, na tulipoteza kasi kidogo,” alisema.

“Lakini basi lazima niseme kwamba tuna bahati sana kuwa na wachezaji wazuri sana ambao wanaweza kuja na kuleta mabadiliko, na Thomas Muller aliingia, Kingsley Coman pia, na wachezaji kutoka benchi walikuwa muhimu sana kwetu kushinda mchezo huu.”

## Barcelona yakanusha Deco kujiuzulu

**BARCELONA,** HISPANIA

BARCELONA imekanusha taarifa zinazodai Mkurugenzi wao wa Soka, Deco anafikiria kujiuzulu wadhifa wake.

Barca wameanza msimu wakiwa katika hali nzuri na kukamilisha ushindi wao wa nne wa La Liga kwenye kampeni Jumamosi usiku huku wakiifunga Real Valladolid mabao 7-0, huku Raphinha akifunga hat-trick.

Hata hivyo, lilikuwa bado dirisha la majira ya kiangazi la ugumu na misukosuko huko Katalunya huku Barca wakiwa bado wanasumbuliwa na masuala ya kiuchumi yaliyoletwa na usimamizi mbaya wa fedha miaka ya nyuma.

Deco alichukua wadhifa wa mkurugenzi wa michezo Agosti mwaka jana na aliweza kutengeneza nafasi ya kutosha katika bajeti kumsajili nyota wa Euro 2024, Dani Olmo, ingawa harakati za klabu hiyo kumnasa Nico Williams hazikufua dafu kwani mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania alibaki Athletic Club.

Presha ambayo imefika na jukumu hilo imeifanya Diario SPORT kudai kiungo huyo wa zamani wa Ureno na Chelsea, anafikiria mustakabali wake Barca.

Migogoro ya ndani, migongano na mawakala na kutoelewana kuhusu msimamo wa klabu katika soko la uhamisho kunadaiwa kuibua mvutano kati yake na Barca.

Hata hivyo, wababe hao wa LaLiga wameondoa uvumi huo, wakielezea ripoti ya SPORT kuwa ni “shambulio”.

Taarifa kutoka kwa klabu hiyo inasomeka: “FC Barcelona inakanusha kabisa habari iliyotokea Septemba Mosi, mwaka huu, kwenye toleo la dijitali la ‘Diario Sport’ na kutilia shaka mwendelezo wa mkurugenzi wetu wa soka.

“Kwa kujibu habari iliyopewa kichwa cha habari cha ‘Deco, amekatishwa tamaa, akitafakari mustakabali wake’, FC Barcelona inasema kwamba haiwezi kuwa na furaha zaidi na kazi inayofanywa na Deco na kukanusha shambulio la ‘Diario Sport’ dhidi ya mkurugenzi wa mpira wa miguu.”



# GAMONDI AFUTA MAPUMZIKO YANGA, BALEKE KIMEELEWEKA

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, ameamua kutovunja kambi, badala yake ameendelea na mazoezi na kikosi kilichobaki, baada ya wachezaji 14 wa timu hiyo kuondoka kwenda kujiunga na vikosi mbalimbali vya timu za taifa kwa ajili ya michezo ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema jana kuwa, awali walidhani anaweza kuvunja kambi na kuwaita baadaye kutokana na kuondokewa na wachezaji wengi, lakini Gamondi amekataa, badala yake ameendelea na wachezaji aliobaki nao kwa ajili ya kujindaa na mchezo wa raundi ya kwanza, Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya CBE ya Ethiopia.

Baada ya Kalenda ya FIFA, klabu nyingi zimewapa mapumziko ya muda mfupi wachezaji wao kabla ya kurejea tena kuendelea na kambi.

"Tupo kwenye mapumziko ya timu za taifa, sisi tumetoa wachezaji 14 kwenda kwenye vikosi vya timu za taifa na tunawatakia kila laheri na waliobaki wanaendelea na mazoezi, baada ya Kalenda ya FIFA kumalizika kutakuwa na siku tatu au nne kabla ya mechi, hivyo kocha hajavunja kambi, wachezaji wanaendelea na mazoezi na wachezaji waliobakia.

Tunaamini tuna kikosi bora hata hawa waliobaki wataandaliwa vema ili waje kungana na wengine watakapotoka kwenye timu zao za taifa kwa ajili ya mchezo wetu muhimu," alisema Kamwe.

Yanga inatarajia kucheza mchezo wa mkondo wa kwanza kwenye Uwanja wa Abebe Bikila nchini Ethiopia dhidi ya wapinzani wao, timu inayomilikiwa na Benki Kuu nchini humo, kabla ya mechi ya marudiano inayotarajiwa kuchezwa, Septemba 20, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kamwe pia alitoa ufafanuzi kwa nini straika mpya wa timu hiyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Jean Baleke, amekuwa haonekani kwenye kikosi hicho, akisema awali tatizo lilikuwa ni vibali, baadaye ikaja changamoto ya Hati ya Uhamisho wa Kimataifa (ITC), lakini kwa sasa limashamalizwa.

"Ni kweli hajaonekana, kwanza kulikuwa na tatizo la vibali, baadaye alikosa mechi mbili za hatua ya awali Ligi ya Mabingwa Afrika, ITC zilichelewa, lakini kwa sasa kila kitu kiko sawa, alikosa mechi ya Kagera kwa sababu ya mahitaji ya kiufundi tu, mwalimu aliona aliosafiri nao wanamtosha kwa mechi ile na si yeye tu aliyebakia Dar es Salaam, ni wengi tu," alisema Kamwe. Hata hivyo, alisisitiza kuwa bado ni mapema sana kwani Yanga ina mashindano mengi na inahitaji wachezaji wengi wenye viwango vya juu, hivyo ana uhakika kuwa atatumika kutokana na mahitaji ya mwalimu.

"Itoshe kusema tuna michezo mingi sana msimu huu na ndiyo kwanza ligi inaanza, inahitajika kuwa na wachezaji wengi wenye uwezo, kwa hiyo anaweza kutumika sana huko mbele ya safari," alisema.

Beleke, awali alikuwa Simba na ilimuacha katikati ya dirisha dogo la msimu uliopita ambapo alitimkia Klabu ya Al Ittihad Tripoli ya Libya kabla ya kuibukia Yanga.

## JKU: Kombe la FA tayari, bado malengo mawili

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya timu ya JKU kutwaa Ngao ya Jamii kwa kuifunga Chipukizi FC mabao 2-0 kwenye mechi iliyochezwa Uwanja wa New Amaan Complex juzi, 'Wajeda' hao wamesema sasa wamebakiza malengo makubwa mawili ndani ya msimu huu 2024-2025 ili kuwa wa furaha zaidi kwao.

JKU ilifanikiwa kutetea taji hilo la Ngao ya Jamii, wakilitwaa kwa mara ya pili mfululizo katika mchezo huo mkali uliopigwa juzi uwanjani hapo.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Kocha wa timu hiyo, Salum Haji, alisema bado mipango yao miwili imebakia ili kuhakikisha msimu huu hawafanyi makosa kama uliopita.

Alisema walichobakisha ni kutetea ubingwa wao wa Ligi Kuu pamoja na kuhakikisha wananyakuwa Kombe la Shirikisho la Soka la Zanzibar, maarufu FA Cup.

Haji alisema mipango yao mikubwa ni kunyakuwa mataji yote matatu na kwamba tayari wameanza na Ngao ya Jamii, hivyo kinachofuata ni kujipanga kwa hayo mawili yaliyosalia.

"Tunaunza msimu kibabe zaidi kama ilivyokuwa kwa msimu uliopita. Msimu huu ni kuhakikisha hakuna tutakachokiacha katika mashindano ambayo tunashiriki," alisema.

Aidha, akizungumzia mchezo huo wa Ngao ya Jamii, alisema haukuwa rahisi, lakini lengo la kutetea taji hilo wamefanikiwa.

Alisema kulingana na uwezo wa kiuchezaji kwa wachezaji wake hana hofu katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar ambayo itaanza rasmi Ijumaa wiki hii.

Alisema kikosi chake kimepata maandalizi ya kutosha kulingana na mashindano waliyoshiriki hasa michuano ya Kombe la Kagame iliyofanyika Tanzania Bara hivi karibuni.

"Mchezo ulikuwa mgumu, lakini wachezaji wangu wamepata uzoefu zaidi, wamecheza kwa mipango na malengo mpaka tumepata ushindi," alisema Haji.

Hata hivyo, alisema licha ya kuwa na wachezaji majeruhi watatu wa kikosi cha kwanza na wanaotegemewa, lakini timu yake ilicheza vizuri na haikuwa na hofu ya mchezo. Kwa mujibu wa ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar iliyotangazwa mwishoni mwa wiki na Bodi ya Ligi visiwani humo, Mabingwa Watetezi, JKU Ijumaa wiki hii watakata utepe wa kinyang'anyiro hicho dhidi ya Wanagenzi Inter Zanzibar ambao wamepanda daraja msimu huu, mchezo ukitarajiwa kupigwa Uwanja wa New Amaan Complex.



Mshindi wa Tuzo ya Kocha Bora wa Agosti, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids.

## Simba, Yanga kutoa mamilioni Taifa Stars

INATOKA UK. 24

lengo walilonalo sasa ni kushinda mchezo huo ili kujiweka kwenye mazingira ya kwenda kucheza tena fainali za AFCON nchini Morocco, kama ilivyokuwa kwa zilizopita nchini Ivory Coast.

"Siku zote jambo lolote ukitaka mwisho wake uwe mzuri ni kufanya mambo mapema, umuhimu wa mechi yetu ni kuanza kushinda na kupata pointi tatu nyumbani ili mbele ya safari tuwe kwenye mazingira rahisi ya kufuzu," alisema.

Hata hivyo, alisema haitokuwa mechi rahisi kwani hata wapinzani wao watakuja wakiwa na akili kama hiyo, hivyo wao makocha na wachezaji itabidi wafanye kazi ya ziada ili kuhakikisha wanafanya kazi kwa vitendo zaidi.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini ( TFF), Cliford Ndimbo, alisema wametangaza viingilio nafuu ili kila Mtanzania apate nafasi ya kuingia uwanjani kuishangilia Stars ambayo imesheheni wachezaji wenye viwango vya juu.

Haji Salum (Mboto), ambaye alizungumza kwa niaba ya wasanii wa bongo muvi, alisema ni wakati wa kudumisha uzalendo na kuachana na mapenzi ya timu.

Msanii wa muziki wa Bongo Fleva, Frank Ngumbuchi 'Foby', alisema kesho ataanza kutoa burudani mapema uwanjani hapo ili wachezaji wapate ari ya kufanya vizuri.

## Fadlu, Ahoua ndio bora zaidi Agosti

INATOKA UK. 24

taratibu wanaanza kuonesha kukaribia apatakapo.

"Najua matarajio ya mashabiki wa Simba, najua nini wanakitaka, tunaenda huko, naamini tutafanya vizuri na kurudisha furaha na matumaini yao," alisema Fadlu.

Alisema katika kipindi hiki ambacho ligi imesimama anaendelea kufanyia kazi kile ambacho anakiona bado hakijakaa sawa ndani ya kikosi hicho.

"Natamani kupata tena mchezo wa kirafiki, uwe wa kimataifa au na timu za ndani, kikubwa ni kuangalia kile tunachokifanya mazoezini kimeshikwa na wachezaji, lakini pia itafanya wachezaji wangu waliopo kwenye kikosi kuendelea kuwa kwenye hali ya kushindana tukiwasubiri wale waliopo kwenye vikosi vya timu za taifa," alisema Fadlu.


Katika hatua nyingine, Fadlu amesema amefurahishwa na viwango vya nyota wake Leonel Ateba na golikipa Aishi Manula ambao walicheza kwa mara ya kwanza Jumamosi chini yake.

Kwenye mechi hiyo, Ateba ndiye alikuwa mfungaji wa bao hilo la Simba huku Manula naye akifanya kazi ya ziada kuokoa michomo kadhaa kabla ya kumpisha Hussein Abel ambaye aliruhusu bao kwa wapinzani wao hao.

Michezo
Jumanne Septemba 3, 2024
Nipashe

Salah: Msimu huu wa mwisho kwangu Liver

UKURASA 21



# Simba, Yanga kutoa mamilioni Taifa Stars

## ●●● Azam nayo ndani, zaungana na Rais Samia kutunisha 'Bao la Mama' zikitaka ushindi wa...

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Klabu za Simba, Yanga na Azam FC, kila moja ikiahidi kutoa Sh. milioni tano kwa Taifa Stars endapo kama itashinda kuanzia mabao matatu dhidi ya Ethiopia kesho kwenye mechi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, naye ataungana nao kwa kutoa kiasi kama hicho lakini yeye ni kwa kila goli ya ushindi.

Taifa Stars itaikaribisha Ethiopia kesho kwenye mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa saa moja usiku, kuwania nafasi hiyo ya kucheza fainali za AFCON zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa hamasa kuelekea katika mchezo huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema Rais Samia ataungana na klabu hizo kutoa zawadi hiyo maarufu kama ‚Goli la Mama'

"Rais Samia ataungana na Klabu za Simba, Yanga pamoja na Azam FC kutoa shilingi milioni tano ya ‚Goli la Mama' kwa kila goli la ushindi litakalofungwa, kwa lengo la kuipa hamasa timu yetu ili ifanye vizuri keshokutwa (kesho)," alisema Msigwa.

Katibu huyo aliwapongeza wasemaji wa klabu hizo kwa ubunifu walioufanya kumuunga mkono Rais Samia kwa kutoa Sh. milioni tano kila moja katika ushindi huo.

Aliwataka wachezaji kupambana na kufuata vema maelekezo wanayoendelea kupewa na benchi lao la ufundi ili wapate pointi tatu, pamoja na kuwaomba Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani hapo.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi uwanjani kuwapa hamasa wachezaji ili waanze vizuri katika mchezo huo wa nyumbani.

"Timu ya Ethiopia haiwezi kutufunga kutokana na kikosi chetu jinsi kilivyo wachezaji wanapaswa kupunguza presha ili waanze vizuri katika mchezo wetu wa kwanza, naamini kila kitu kinawezekana," alisema Ally.

Kwa upande wa Meneja wa Habari wa Klabu ya Yanga, Ally Kamwe, aliwaomba Watanzania kununua tiketi kwa wingi ili wakajaze uwanja.

"Msimu huu nimekuja na wazo jipya kwa upande wa hizi klabu tatu kila moja itatoa milioni tano kwa ajili ya kumuunga mkono Rais Samia katika hamasa yake ya Goli la Mama," alisema Kamwe.

Hata hivyo, Msemaji wa Azam FC, Hashim Ibwe alisema kundi la Stars si gumu, hivyo ina uwezekano mkubwa wa kupata ushindi endapo mashabiki watajaza uwanja," alisema Ibwe.

Wakati huo huo, Kocha Msaidizi wa Taifa Stars, Juma Mgunda, alisema kikosi hicho sasa kimeiva na kipo tayari kuivaa Ethiopia kesho kwenye mchezo huo wa kwanza wa Kundi H, kusaka tiketi ya kufuzu kucheza fainali za Mataifa ya Afrika.

Akizungumza kwenye mazoezi ya timu hiyo yanayofanyika kwenye Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam, Mgunda alisema wachezaji wameimarika kwa asilimia 80, na kilichobaki ni kumalizika asilimia zilizosalia ili wawe fiti asilimia 100.

"Tumeandaa kikosi na wachezaji wako fiti kwa asilimia 80, na tunamalizia siku zilizobaki ili tuwe na asilimia 100 ya kuivaa Ethiopia, tumekuwa tukizungumza na vijana juu ya kuwa na utayari wa kuitetea nchi yao na kuiwakilisha vizuri, wanaonekana wako vizuri na tayari kwa mechi hiyo," alisema Mgunda.

Akiizungumzia mechi hiyo, alisema

INAENDELEA UK. 23

# Fadlu, Ahoua ndio bora zaidi Agosti




Mchezaji Bora wa Agosti, Kiungo wa Simba, Jean Charles Ahoua.

**Na Faustine Feliciane**

HUKU Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, akisema ana matumani makubwa na kikosi hicho kwenye michuano yote ikiwamo Kombe la Shirikisho Afrika na kwamba ni suala la muda tu kabla hawajaanza kuonesha makali yao, amefungua msimu wa Ligi Kuu Bara kwa kuwa mwalimu wa kwanza kutwaa tuzo ya Kocha Bora wa Mwezi Agosti yeye pamoja na Kiungo wa timu hiyo, Jean Charles Ahoua.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi jana, imeeleza kuwa Fadlu ametwaa tuzo hiyo kutokana na kuiwezesha Simba kushinda mechi mbili ndani ya mwezi huo baada ya kuichapa Tabora United mabao 3-0 na kisha kupata ushindi wa 4-0 dhidi ya Fountain Gate.

Katika kinyang'anyiro hicho, Fadlu amewashinda Patrick Aussems wa Singida Black Stars na Abdallah Mohamed wa Mashujaa FC.

Kwa upande wa Ahoua ametangazwa kuwa mchezaji bora wa mwezi huo baada ya kuisaidia timu hiyo kuvuna alama hizo saba kwa kufunga bao moja na kuhusika katika mabao mengine matatu.

Kikosi hicho cha Simba, pia Jumamosi iliyopita kilicheza mchezo wa kimataifa wa kirafiki dhidi ya Al Hilal ya Sudan na kutoka sare ya bao 1-1.

Fadlu, alisema taratibu mfumo wake unaanza kuwaingia wachezaji wake na muunganiko aliokuwa akiutaka ameanza kuuona.

Fadlu, alisema bado timu haijafika pale anapopataka, lakini

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >